





UKURASA 5

## TMDA yafanya utafiti dawa za kuongeza nguvu za kiume nchini




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Julai 10, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581002

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# PID; ugonjwa unaotesa wanawake kimyakimya



**WANAUME** sehemu ya tatizo... *Endelea ukurasa 4*



Waislam wa dhehebu la Answar al-Sunna, wakiswali ibada ya Eid El Hajj katika Uwanja wa Jitegemee, wilayani Muheza, mkoani Tanga jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Ulevi, uvivu vilivyo chanzo cha umaskini katika familia

UKURASA 8

UKURASA WA 2

### NEC YATEUA MBUNGE

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imemteua Tamima Abass kuwa...

UKURASA WA 3

### VIGOGO WAZIDI KUJITOSA KATIKA UCHAGUZI CCM

MWANASIASA James Lembeli aliyewahi kuwa Mbunge wa...

UKURASA WA 11

### UMEOLEWA KUMBE MCHUMBA WA KWANZA BADO ANAKUHITAJI

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na simulizi ya kijana...

## Bosi wa UN ahimiza kasi uchanjaji wa UVIKO-19

UKURASA 5

**MICHEZO** BI. HINDU KUZIKWA LEO, SIMBA, WASANII WAMLILIA UK. 23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia amlilia Dos Santos

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, ametuma salamu za rambirambi kwa Mwenyekiti wa Chama cha MPLA na Rais wa Angola, Komredi João Manuel Gonçalves Lourenço kufuatia kifo cha aliyekuwa mwenyekiti wa chama hicho, José Eduardo dos Santos, aliyefariki dunia juzi.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, ilibainisha kuwa Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia amepokea kwa masikitiko taarifa za kifo hicho.

Alisema Dos Santos alikuwa mmoja wa viongozi wa kikosi kilichoshiriki ukombozi wa nchi za Bara la Afrika, wakiongoza mapambano ya mataifa kujikomboa kutoka utawala wa kikoloni.

"Dos Santos ni kiongozi shupavu aliyeongoza MPLA kulinda uhuru wa nchi yake na watu wake dhidi ya mashambulio ya wapinga uhuru.

"Chama Cha Mapinduzi kinakumbuka na kuthamini mchango wa Komredi José, ambaye kwa kushirikiana na viongozi wenzake wa mapinduzi Afrika, miongoni mwao Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Angola, Komredi Agostinho Neto na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, waliona umuhimu wa kushirikiana kusaidia mapambano ya uhuru wa nchi zingine zilizokuwa bado katika minyororo ya wakoloni, hususani za kusini mwa Afrika," alisema.

Katika salamu hizo, Rais Samia alisema CCM itamkumbuka Komredi Dos Santos kama kiongozi wa kuigwa aliyependa nchi yake kwa uzalendo mkubwa.

"Kupitia uongozi wake kwa MPLA, chama hicho imara kiliweza kuiongoza na kuisimamia Jamhuri ya Angola kuendelea kuwa taifa moja kwa maslahi ya wananchi.

"Mbali na kukiongoza chama cha MPLA na Jamhuri ya Angola kikamilifu katika kulinda uhuru dhidi ya matishio ya ndani na nje, Komredi Dos Santos, alishirikiana na viongozi wenzake katika mapambano ya kuzikomboa nchi za Afrika kiuchumi," alisema.

Pia alisema ushirikiano wao ulikuwa msingi wa kuanzishwa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), ambayo wanajivunia umuhimu wake na matunda yake wakati huu.

Mwenyekiti huyo wa CCM alisema kuwa kutokana na mchango wake katika harakati za ukombozi wa mataifa ya Kusini mwa Afrika na Afrika kwa ujumla pamoja na maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa watu katika nchi, msiba huo siyo wa Jamhuri ya Angola pekee.

"Msiba huu siyo wa Jamhuri ya Angola pekee, bali ni wetu sote, ni huzuni kubwa kwetu sote," alisema Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia.



Mbunge wa Jimbo la Peramiho, ambaye pia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, akishiriki kufyatua tofali za mradi wa kikundi cha vijana wa Kijiji cha Mpangula, Kata ya Matimira, akiwa katika ziara yake mkoani Ruvuma jana, iliyolenga kuhimiza ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NEC yateua mbunge wa viti maalum

**Na Romana Mallya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imemteua Tamima Abass kuwa Mbunge wa Viti Maalum kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Uteuzi huyo umefanyika kutokana na kifo cha Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa, Irene Ndyamkama, aliyefariki dunia Aprili 24 mwaka huu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani (Tumbi) iliyoko Kibaha kwa matatizo ya uzazi.

Mkurugenzi wa Uchaguzi NEC, Dk. Wilson Charles, katika taarifa yake aliyoitoa jana kwa vyombo vya habari, alisema katika kikao kilichofanyika jana, tume kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 78 (4) ya Katiba ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 86A(6) na (8) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, imemteua Tamima kuwa mbunge.

"Uteuzi huu umefanyika baada ya tume kupokea barua Mei 12 mwaka huu, yenye kumbukumbu namba CEB.137/400/02A/10 kutoka kwa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, iliyoandikwa kwa mujibu wa kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi.

"Sura ya 343 ikitaarifu kuhusu kuwapo nafasi ya Mbunge wa Viti Maalum wa CCM kutokana na kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Irene Ndyamkana," alisema.

Irene alifariki dunia siku hiyo katika hospitali wakati akipatiwa matibabu na kuacha mtoto ambaye naye alifariki dunia siku saba baadaye.

# Bil. 2.6/- zatengwa upanuzi wa uwanja

**Na Mwandishi Wetu**, LINDI

SERIKALI imetenga fedha za ndani Sh. bilioni 2.6 kwa ajili ya kuanza taratibu za kuwapata makandarasi wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege Lindi.

Akizungumza baada ya kutembelea uwanja huo jana, Naibu Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema serikali imedhamiria kuwezesha miundombinu ya viwanja vya ndege, barabara na bandari kama mkakati wa kuiwezesha miradi mikubwa inayotarajiwa kuanza kutekelezwa mkoani humo.

"Serikali hii chini ya uongozi wa Rais Samia imeshaelekeza maboresho ya miundombinu ya kimkakati katika mkoa huu yafanyike haraka kama ilivyopangwa mkoani na isipate changamoto yoyote ile," alisisitiza.

Naibu Waziri Mwakibete aliutaka Wakala wa Barabara (TANROADS) na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kuhakikisha michoro ya kiwanja hicho inazingatia uhalisia wa aina ya miradi ya kimkakati ili kutorudia kazi hiyo.

Mbunge wa Lindi Mjini, Hamida Abdallah, aliishukuru serikali kwa uamuzi wa kuanza mchakato wa kuboresha kiwanja hicho na kusema kuwa kukamilika kwa kiwanja hicho kutatochea ukuaji wa uchumi wa mkoa na kuibua fursa mbalimbali zilizopo.

Mhandisi wa Matengenezo ya Viwanja vya Ndege kutoka TANROADS Mkoa wa Lindi, Ezra Magogo, alisema kwa sasa wakala uko kwenye hatua za kupitia michoro iliyopendekezwa na akamhakikishia naibu waziri huyo kuwa watazingatia maboresho kwa kuwa michoro iliyowasilishwa kwa sasa imezingatia ndege zenye uwezo wa kubeba abiria takriban 70.

Awali akitoa taarifa ya kiwanja hicho, Mkurugenzi wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa kutoka TAA, Hamisi Amiri, alisema mamlaka hiyo na TANROADS zinaendelea kushirikiana kwa karibu kuhakikisha maboresho yanayofanyika kuanzia ngazi ya michoro mpaka kufikia utekelezaji kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) ili kuhakikisha viwango vinazingatiwa.

Kiwanja cha Ndege cha Lindi kwa sasa kinapokea ndege zisizo za ratiba na kwa mwaka 2021/22 kimeweza kuhudumia abiria zaidi ya 1,000 na ndege zaidi ya 100.

# HABARI KITAIFA



Mkazi wa Pugu Kinyamwezi, jijini Dar es Salaam, Aldo Adani, akionyesha kwa waandishi wa habari juzi, eneo la kiwanja anachodai kuwa ni chake na kimevamiwa na mtu asiyemjua na kujenga nyumba inayoonekana ya rangi nyeupe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Vigogo wazidi kujitosa katika uchaguzi CCM

**Na Waandishi Wetu**

MWANASIASA James Lembeli aliyewahi kuwa Mbunge wa Kahama kuanzia mwaka 2005 hadi 2015 kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), baadaye akajiunga na CHADEMA na kurejea tena CCM, amechukua fomu ya kugombea nafasi ya Uenyekiti CCM Mkoa wa Shinyanga.

Lembeli alichukua fomu hiyo jana kwenye Ofisi za CCM Mkoa wa Shinyanga na kukabidhiwa na Katibu wa chama hicho mkoa, Donald Magesa.

Akizungumza wakati wa kuchukua fomu hiyo, Lembeli alisema ameamua kugombea nafasi hiyo baada ya kujipima na kujitathimini na kujiona kuwa nafasi hiyo anaiweza kutokana na uzoefu wake ndani ya chama, pia ni kiongozi mzoefu ndani na nje ya nchi.

Lembeli ambaye amewahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira (2010-15), alisema CCM Mkoa wa Shinyanga inahitaji viongozi thabiti, makini na wasiokuwa na 'makandokando', sifa ambazo alisisitiza anazo. "Nimejipima na kujitathimini nikaona nije nichukue fomu ili nigombee nafasi ya Uenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga kwa sababu sifa zote ninazo, hasa katika zama hizi ambapo kuna changamoto nyingi," alisema Lembeli.

Julai 6 mwaka huu, aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga kuanzia mwaka 2007 hadi 2015 kisha akahamia CHADEMA na kurudi CCM, Hamis Mgeja, alichukua fomu ya kugombea tena nafasi hiyo.

Katibu wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Magesa, alisema idadi kamili ya wagombea wote ambao wamechukua fomu itatangazwa leo, ambayo ni siku ya mwisho kwa uchukuaji fomu.

Wakati hali ikiwa hivyo mkoani Shinyanga, wilayani Kibiti mkoani Pwani, wanachama 85 wa CCM wamejitokeza kuchukua fomu za kuwania nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama hicho.

Wanachama hao ni pamoja na Mwenyekiti wa CCM Wilaya hiyo anayemaliza muda wake, Jabir Marombwa.

■**Imeandaliwa na Marko Maduhu (SHINYANGA) na Julieth Mkireri (KIBITI).**

## Kilombero kuongeza uzalishaji wa sukari

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Uzalishaji Sukari ya Kilombero inatarajia kuanza kuzalisha tani 270 kwa mwaka kutoka uzalishaji wake wa sasa wa tani 130 kwa mwaka.

Kampuni hiyo yenye chapa ya Bwana Sukari inajenga kiwanda kingine chenye uwezo wa kuzalisha tani 140 kwa mwaka.

Mkurugenzi wa Biashara Afrika wa Kampuni ya Kilombero, Andre Lube, alibainisha hayo jana katika banda lao lililoko katika viwanja vya Maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara, maarufu Sabasaba, alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema wako Sabasaba kwa ajili ya kuonyesha bidhaa zao na kuuza sukari kwa washiriki wa maonyesho hayo na lengo kubwa la kampuni hiyo ni kutoa huduma kwa Watanzania wengi.

"Ninamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha sekta ya viwanda nchini ili kuongeza kiwango cha ajira kwa vijana na kukuza uchumi wa Taifa letu.

"Kilombero tumejipanga kuongeza uzalishaji sukari kwa kuanzisha kiwanda tunachojenga ili kufikia tani 270 kwa mwaka," alisema Lube.

Alisema bidhaa hiyo imekuwa ikizalishwa na Watanzania wenyewe na kuuzwa kwa Watanzania hivyo kukuza uchumi wa nchi kwa kiwango kikubwa.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo, Guy William, aliishukuru serikali kwa kurahisisha mazingira ya uwekezaji na kuahidi kuzalisha bidhaa zenye ubora wa hali ya juu.

"Ninaona fahari kuwa mwekezaji wa kiwanda cha Kilombero katika kuhakikisha Watanzania wote wanatumia bidhaa ya sukari inayozalishwa Tanzania na Watanzania," alisema William.

## Mpima ardhi kizimbani kwa mashtaka hasara mamilioni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma imemfikisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma, Mpima ardhi Charles Fungo, mkazi wa Dar es Salaam, akikabiliwa na mashtaka ya kuisababishia hasara ya Sh. milioni 10.8 Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Mshtakiwa huyo anadaiwa kutenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Leonard Haule, alidai kuwa katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi namba 2/2022, Fungo alitumia mamlaka aliyokuwa nayo kujipatia fedha hizo badala ya kuzitumia katika ujenzi wa minara kwenye Kijiji cha Veyula jijini Dodoma. Baada ya kusomewa mashtaka hayo, mshtakiwa alitakiwa kutekeleza masharti ya dhamana lakini hakuyatimiza, hivyo kupelekwa rumande.

Shauri hilo litatajwa Julai 18 mwaka huu kwa ajili ya kuanza kusikilizwa kwa hoja za awali kwa pande zote mbili katika mahakama hiyo.

Mbali na hilo, TAKUKURU wilayani Kondoa imewafikisha mahakamani waliokuwa viongozi wa Kijiji cha Madege kwa mashtaka ya kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni mbili pamoja na ubadhirifu wa mali ya umma.

Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU aliwataja waliofikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kondoa mbele ya Hakimu Mwajuma Lukindo kwa shauri la uhujumu uchumi namba 6/2022 ni: Bashiru Dina, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Madege; Mustapha Njoro, aliyekuwa Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Madege; Omary Mafita, Kassim Msengi na Abdalah Abdalah ambao wote walikuwa wajumbe.

Kwa mujibu wa Haule, shauri hilo lilifunguliwa Juni 29 mwaka huu mbele ya Hakimu Mwajuma Lukindo wa Mahakama ya Wilaya ya Kondoa ambapo washtakiwa watano wanadaiwa kutumia fedha za Kijiji cha Madege tofauti na maelekezo ya matumizi ambayo yalitakiwa kufanyika ikiwamo kutekeleza mambo mbalimbali ya maendeleo ya kijiji hicho.

Haule alisema kuwa baada ya TAKUKURU kupata taarifa, walifanya uchunguzi katika kijiji hicho na kubaini kuwapo ubadhirifu na ufujaji wa fedha hizo.

Hata hivyo, washtakiwa waliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti yaliyotakiwa na kuongeza kuwa washtakiwa hao wanatakiwa kuwapo mahakamani Julai 12 mwaka huu, shauri lao litakapotajwa.

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(TEMEKE HIGH COURT SUB-REGISTRY)**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTER)**
**AT TEMEKE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.48 OF 2022**

**In the matter of the estate of the late PATRICIA FORTUNATA MWANUKUZI**

**AND**

**In the matter of administration by MARGARET MALWA BANDORA**

**NOTICE TO CREDITORS**

**(RULE 111)**

**NOTICE** is hereby given that, all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above named **PATRICIA FORTUNATA MWANUKUZI** deceased, who died at Dar es salaam on the 13th day of may,2020 and probate of whose letters of administration was granted to me by the court on the 25th day of may 2022,are hereby required to send in their claims to me at the following address **'MARGARET MALWA BANDORA P.O.BOX 3457,DAR ES SALAAM '** within **60** days from the date of the publication of this notice at the expiration of which time I shall proceed to hand over the asset to the persons entitled there to having regard only to the claims of which I shall then have had notice.

**Margaret Malwa Bandora**
**(Administratrix)**

116938802



# PID; Ugonjwa unaotesa wanawake kimyakimya

**Na Waandishi Wetu**

PID ni kifupisho cha Pelvic Inflammatory Disease. Kwa lugha yetu ya Taifa ni maambukizo katika mfumo wa uzazi wa mwanamke. Ni ugonjwa unaotajwa kuwasumbua vijana wengi kwa sasa.

Kundi kubwa la waathirika wa ugonjwa huo ni wanawake wenye miaka kati ya 18 na 25, ambao wamekuwa wakiteseka na ugonjwa huu bila kupata msaada na wengi hawana uelewa wowote kuhusiana na PID.

Kwa kutokuwa na uelewa huo, wengi huogopa kwenda hospitalini kwa kuona aibu na madhara yake yanakuja kuwa makubwa mbeleni, yakijumuisha kushindwa kupata ujauzito na ujauzito kuharibika.

Wataalamu wanabainisha kuwa kwa kawaida maambukizo yanahusisha shingo ya kizazi (cervix), kitaalamu ikijulikana kama cerviatis, nyama ya mfuko wa uzazi (endometritis) na mirija ya uzazi (salphingitis).

Kwa mujibu wa chapisho la mwaka 2022 la Chama cha Kisukari cha Amerika (ADA 20220), PID ni maambukizo ya via vya uzazi vya mwanamke yakijumuisha maambukizo ya bakteria kwenye shingo ya uzazi, mirija ya fallopio, ovari na tumbo la uzazi (uterasi).

ADA wanasema kuwa sababu kuu ya ugonjwa huo ni maambukizo yanayosambazwa kwa kujamiiana (STI). Ugonjwa huo unaweza kuwaathiri wanawake wenye umri wowote, lakini wale wenye umri kati ya maika 15 na 24 huathirika zaidi.

Kwa mujibu wa tovuti ya Lindaafya.com, wataalamu wa afya wanaamini magonjwa ya zinaa ambayo hayakutibiwa ipasavyo, hasa kisonono (gonorrhea) yanaongoza kwa kusababisha PID.

"Kuna baadhi ya wanawake wanaugua PID pasipo magonjwa ya zinaa. Pengine kutokana na maambukizo ya kawaida ya bacteria (bacteria vaginosis)," inafafanuliwa zaidi katika tovuti hiyo.

Pia kuna angalizo la kitabibu kwamba, unaweza kujitambua mwenyewe kama umeathirika na ugonjwa wa PID kwa kurejea historia ya kupata maambukizo ya mfumo wa haja ndogo (UTI) na umeitibu kwa dozi sahihi kwa muda mrefu bila mafanikio.

Vilevile, kama umetumia dawa za kupachika sehemu za faragha kwa lengo la kutibu fangasi au UTI kwa muda mrefu na unapona, lakini tatizo linarudia kila mara, ujue kuwa umeathirika na ugonjwa huu wa PID.

Hadhari pia inatolewa kwa mtu mwenye matatizo ya magonjwa ya zinaa, lakini anatokwa uchafu wenye rangi nyeupe, njano, kijani ama majimaji yanayotoa harufu kali kutoka sehemu za faragha, basi naye atambue yuko hatarini kwa PID.

Daktari Yunus Mohamed kutoka Kampuni ya BF SUMA Arusha, anaeleza dalili za ugonjwa huo zinazoonekana mapema na zilizojificha, akifafanua:

"Mwanamke anapokuwa na PID, huwa anatokwa na uchafu sehemu za siri kulingana na aina ya maambukizo. Anaweza kuwa na ... (alitamka neno lenye maana ya ute unaotoka sehemu za faragha za mwanamke) wa rangi nyeupe, njano au kijani na muda mwingine kahawia, ukiambatana na harufu mbaya.

"Pia maumivu ya tumbo chini ya kitovu lakini pia kuhisi maumivu wakati wa kujisaidia haja ndogo, mwili kuchoka, kichefuchefu, kupoteza hamu ya kula na kuna baadhi ya watu wanapata maumivu wakati wa tendo la ndoa, maumivu wakati wa hedhi na baadhi yao hedhi huwa inagoma au kuona hedhi mfululizo.

"UTI inapokuwa sugu inapelekea maambukizo ya bakteria wanaoweza kuhama kutoka kwenye njia ya mkojo kwenda kwenye njia ya uzazi, hapo ndipo maambukizo ya PID yanatokea.

"Kama hawajahama, hubaki kuwa UTI, lakini mara nyingi ikiwa sugu, wale bakteria wanaenea eneo kubwa, kwa maana njia ya mkojo na njia ya uzazi ni jirani."

Mtaalamu huyo anabainisha kuwa upo uwezekano mkubwa wa wanawake kupona PID, lakini wengi wao wako hatarini kupata maambukizo tena kutokana na kuishi kwenye visababishi vya ugonjwa huo, hivyo muhimu kwao ni kutambua visababishi ili kujikinga na ugonjwa huo.

"Ugonjwa wa PID unakuwa kwa kasi kubwa sana na baadhi ya wanawake hupata madhara makubwa baadaye hususani ugumba, saratani ya kizazi, harufu mbaya sehemu za siri, kutokwa na majimaji, mirija ya uzazi kuvimba na kuziba na mzunguko wa hedhi kuharibika na mimba kuharibika kutokana na kupuuzia matibabu ya ugonjwa huu.

"Na ikiwa unaona dalili za ugonjwa huu jitahidi kuanza matibabu kabla hujapata madhara ambayo yanaweza kugharimu maisha yako kwa ujumla," Dk. Mohamed anatahadharisha.

Mshauri wa Masuala ya Afya na mkazi wa Dar es Salaam, Prince Mosses, anawasilisha uzoefu wake katika eneo hilo, akiweka bayana kwamba wanawake wengi wanateseka na shida hiyo.

Anafichua maficho mengine kwa baadhi ya wanawake kupata ugonjwa huo mara kwa mara kutokana na matibabu kutofanyika kwa wenzi wao.

"Wanawake wengi wanatibiwa ugonjwa huu peke yao na kusahau kuwa ukitibiwa wewe, inabidi mpenzi au mume wako pia atibiwe. Usipofanya hivyo, basi utakuwa unarudi tena na tena.

"Matumizi ya antibiotic yanakufanya zile dalili zote zinapotea na kukufanya uamini kuwa ugonjwa huisha mara moja. Kwa hiyo, baada ya muda kupita, dalili zinaanza tena na ugonjwa unajirudi.

"Sababu nyingine ni kinga za mwili kushuka kutokana na mazingira unayoishi, vyakula tunavyokula ukizingatia vina kemikali nyingi, miili yetu inashindwa kutengeneza kinga madhubuti ya kupambana na magonjwa.

"Kwa hiyo, ukitibiwa na mwili ukiwa hauna kinga imara, ni rahisi kupata maambukizo ya magonjwa mbalimbali," Mosses anahitimisha.

Dk. Dominic Nachunga wa magonjwa ya wanawake kutoka KBD Polyclinic Kijitonyama mkoani Dar es Salaam, anaungana na wataalamu wenzake kupaza sauti dhidi ya ugonjwa huo, akisema athari zake ugonjwa mbali na kusababisha ugumba wa kudumu na maumivu makali ya tumbo, pia husababisha mimba kutungwa nje ya kizazi.

Anawataka vijana kuwa makini na ugonjwa huo kwa kuwa waaminifu kwa wenzi wao na kuzingatia matibabu ya pamoja pale mmoja anapobainika kuwa na vimelea vya ugonjwa huo.

Daktari huyo pia anawataka wanawake kuwa makini katika usafi wa via vya uzazi kwa kuepuka kutumia dawa zenye kemikali kama vile sabuni na kuwa makini na mikono yao wanaposafisha maeneo yao ya faragha.

■**Imeandaliwa na Aisha Mbuma na Milembe Mipawa (SJMC).**



# Mwitikio wa wananchi utalii Sabasaba waikosha TANAPA

**Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limesema mwitikio wa wananchi katika banda la Maliasili na Utalii kwenye maonyesho ya kimataifa ya 46 ya Biashara Dar es Salaam 'Sabasaba' umekuwa chachu ya kufikisha elimu juu ya vivutio vya utalii.

Ofisa Mwandamizi wa TANAPA Kitengo cha Maendeleo ya Biashara, Enice Msangi, alibainisha jana mkoani Dar es Salaam kuwa mwitikio wa wananchi umekuwa mkubwa katika banda hilo ambalo pamoja na kupata fursa ya kushuhudia vivutio mbalimbali, pia wamepata maelezo sahihi kuhusu uhifadhi na vivutio vya utalii nchini.

Alisema hamasa ya wananchi waliojitokeza kwenye maonyesho hayo ya kutaka kufahamu kwa kina kuhusu masuala ya utalii nchini, imekuwa chachu kwa sekta hiyo kuzidi kukua na kuendeleza juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan katika kutangaza utalii.

"Wananchi wamehamasika sana kutaka kupata taarifa zaidi za masuala ya utalii, wengi tumekuwa tukiwaelimisha na kuwapa taarifa pia kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo katika hifadhi zetu tano mpya kati ya 22 zilizopo nchini, uwekezaji ambao utafanyika bila kuleta uharibifu katika ikolojia au mazingira ya hifadhi," alisema Eunice.

Alisema pia kuna ofa za utalii ambazo wameziandaa wakishirikiana na wadau wengine wa utalii kama Nesa Africa, hivyo wananchi watajiandikisha kwa ajili ya ofa hizo na zoezi ni endelevu kwenye viwanja vya Sabasaba hadi maonyesho yatakapofungwa.

"Kwenye banda la Maliasili na Utalii kuna vivutio vingi ambavyo kwa atakayebahatika kulitembelea, atajiona wa tofauti kwenye utalii, ingawa kwa upande wetu TANAPA, mbali na kupata elimu na taarifa za ofa za utalii, pia utakapotembelea banda letu utapata historia ya hifadhi zote 22 za taifa.

"Tunatoa historia ya mali kale zinazosimamiwa na TANAPA kama vile nyumba ya kumbukizi ya Mwalimu Nyerere ya Magomeni, Dar es Salaam, Isimila Guruneti iliyopo Iringa, Kituo cha Dk. Living Stone, Kigoma na Caravani Serai kilichoko Bagamoyo ambacho kina historia ya msafara wa watumwa," alisema.

Akizungumzia mwitikio wa wananchi kwenye gari aliloendesha Rais Samia wakati wa kuandaa filamu ya Tanzania The Royal Tour ambalo lipo kwenye banda hilo kama moja ya vivutio, Eunice alisema tangu limepelekwa kwenye maonyesho hayo, mwitikio wa wananchi kwenda kuligusa na kupiga nalo picha umekuwa mkubwa.

Kwenye banda la Maliasili na Utalii katika Viwanja vya Sabasaba, kuna wanyama kama simba, chui, chatu, mamba, nyoka na fisi.



Baloziwa Canada hapanchini Pamela O'Donnell (katikati) akijadiliana jambo na Meneja Uendeshaji wa kampuni ya Pan African Energy Tanzania, Peter Sololo wakati wa maadhimisho ya siku ya Canada, nyumbani kwa balozi, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kushoto ni Meneja Lojistiki wa kampuni hiyo, Stella Ndossi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TMDA yafanya utafiti dawa kuongeza nguvu za kiume

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imesema inafanya utafiti wa dawa za nguvu za kiume aina ya Viagra kwa kuangalia matumizi yake na idadi ya watumiaji ili itoe elimu sahihi kwa jamii.

Vilevile, imesema imeweka mkakati dhidi ya dawa aina ya P2 kwa lengo la kudhibiti matumizi holela kutokana na kubainika kutumiwa zaidi na wanafunzi wengi kwa lengo la kuzuia mimba.

Mkurugenzi wa TMDA, Adam Fimbo, alibainisha hayo juzi mkoani Dar es Salaam katika Maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara, maarufu kama Sabasaba.

"Matumizi ya dawa za Viagra yamekuwa makubwa nchini na tunafanya utafiti kuangalia matumizi yake kwa ukubwa yapo kwa kiwango gani, lengo ni kutoa elimu zaidi kwa wale ambao wanatumia visivyotakiwa, kwa sababu kuna matukio mengi ya watu kupoteza maisha kwa kupata shinikizo la damu," alisema.

Fimbo alisema utumiaji holela wa dawa za jamii ya kutolewa mimba na za kuongeza nguvu za kiume umekuwa ukisababisha madhara kwa watu.

Aliongeza kuwa dawa ni bidhaa za sumu, hivyo hazitakiwi kutumika kiholela na ni muhimu kabla ya mtu kutumia dawa, apime na kufuata ushauri wa daktari.

"Tupo hapa Sabasaba kuyaeleza haya ili wengi wafahamu kuwa dawa ni hatari kwa afya zao, hivyo ni muhimu kabla hujazitumia, kwanza ukapimwe kama unaumwa na kufuata ushauri wa daktari.

"Tumekuwa tukipata ripoti mbalimbali kwamba watu wengi wamepoteza maisha na wengine kupata shinikizo la damu, hivyo wito wangu ni kwamba tusitumie dawa hizi bila kufuata ushauri wa wataalamu," alisema.

Fimbo alisema kwa upande wa dawa za P2 , nazo zimekuwa zikitumiwa na wanafunzi kuzuia kupata ujauzito.

"Tumeweka mkakati wa kuhakikisha tunatoa elimu kwa watoto wetu wa kike na wanawake kuacha kutumia dawa hizi kiholela kwa sababu zinasababisha vifo visivyotarajiwa na kuelimisha jamii matumizi sahihi," alisema.

Sambamba na hilo, Fimbo alisema wameweka mfumo wa ukaguzi kila siku katika maeneo mbalimbali ikiwamo bandarini.

Alisema dawa bandia ni dawa zilizotengenezwa kwa makusudi ya kudanganya au kuficha uhalisia wake kwa njia ya vifungashio au viambata vinavyotumika.

"Kazi yetu kubwa ni kuzikamata na matukio kama haya yapo na endapo tukibaini tunawakamata tunafanya ukaguzi na kushirikisha Jeshi la Polisi," alisema.

# Bosi UN ahimiza kasi chanjo corona nchini

**Na Getrude Mbago**

KATIBU Mkuu Msaidizi wa Umoja wa Mataifa na Mratibu Kiongozi wa Kimataifa wa Ushirikiano wa Utoaji Chanjo ya UVIKO-19 (CoVDP), Ted Chaiban, amehitimisha ziara ya siku nne nchini na kutoa wito kwa Tanzania kuendeleza kasi katika utoaji wa chanjo ya ugonjwa huo.

Akizungumza katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam juzi, alipotembelea kwa mwaliko wa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, Chaiban alisisitiza dhamira ya Umoja wa Mataifa na jumuiya ya kimataifa kwa ujumla kushirikiana na Tanzania ili kuendeleza kasi iliyojengeka ya utoaji wa chanjo ili kulinda afya za wananchi.

Akiwa na mwenyeji wake, ofisa huyo wa Umoja wa Mataifa alitembelea mabanda kadhaa, likiwamo la burudani, ambapo wanamuziki maarufu na nyota wa filamu walikutana na mashabiki wao.

"Tanzania imefanya kazi kubwa kwa kuongeza ushamiri wa chanjo kutoka asilimia sita wiki chache zilizopita hadi zaidi ya asilimia 12 sasa," alisema.

Chaiban aliongeza: "Kama chanjo itaendelea kwa kasi hii ya sasa, nchi hii inaweza kufikia lengo lake la kuchanja asilimia 70 ya watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea kufikia Desemba mwaka huu."

Waziri Ummy alisema kampeni ya utoaji chanjo iliyozinduliwa mwezi Juni mwaka huu, imeleta mafanikio makubwa kulinganisha na zile zilizotolewa kwa miezi tisa iliyopita.

"Tumeona ongezeko kubwa la idadi ya waliochanjwa kuanzia Mkoa wa Ruvuma ambao ulipeleka chanjo karibu zaidi na jamii tangu awali. Kwa hiyo, tulipitisha rasmi mbinu hiyo na kuweka malengo kwa kila mkoa.

"Wizara yangu itahakikisha kwamba msaada unaopatikana kwa washirika unatumika kwa ufanisi kupitia mfumo wetu wa tawala za mikoa hadi ngazi ya vituo vya afya," alisema.

Waziri huyo alisema ofisi ya Shirika la Afya Duniani nchini imekuwa ikisaidia juhudi za chanjo kupitia msaada wa kiufundi na kifedha katika kupanga mipango ya chanjo ngazi ya mikoa na wilaya, ufuatiliaji na usimamizi wa takwimu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Suala la Katiba Mpya lisitawaliwe na siasa

**KATIKA** siku za hivi karibuni, kumekuwa na shinikizo kutoka makundi mbalimbali yakiwamo vyama vya siasa, asasi za kiraia, wasomi na watu waliowahi kushika nyadhifa mbalimbali katika mihimili ya serikali, kutaka kufufuliwa kwa mchakato wa Katiba Mpya pamoja na Tume Huru ya Uchaguzi.

Watu hao wanataka mchakato huo uanze mapema licha ya kwamba serikali ilishaunda kikosi kazi ambacho kinaratibu maoni mbalimbali kwa ajili ya kupatikana kwa maridhiano ya kisiasa, ikiwa ni njia ya kurejesha uhusiano baina ya serikali, chama tawala - Chama Cha Mapinduzi (CCM) na vyama vya siasa. Hatua hiyo inatokana na kutokuwapo kwa maelewano mazuri baina ya serikali na wadau wengine wakiwamo vyama vya siasa na wanaharakati.

Baadhi ya makundi hayo, yanataka mchakato huo uanze mapema ikiwezekana Oktoba, mwaka huu ilhali serikali imesema suala hilo linahitaji subira sambamba na kupatikana kwa taarifa ya kikosi kazi kilichoundwa.

Pamoja na kuwapo kwa madai hayo, CCM kwa upande wake imeweka wazi kwamba suala hilo liko wazi na kwamba ni mahitaji muhimu ya wakati wa sasa, isipokuwa linahitaji utulivu katika kulifanikisha.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, juzi aliweka tena bayana suala hilo alisema suala hilo ni mwendelezo wa yale yaliyofikiwa katika lililokuwa Bunge Maalum la Katiba, hivyo hakuna haja ya watu kupaza sauti kwa kuwa muda ndio utakaoamua.

Licha ya kuzungumzia Katiba Mpya, pia aliweka bayana kwamba hata suala la Tume Huru ya Uchaguzi nalo halina budi kusubiri hadi kikosi kazi kimalize kazi yake ya kukusanya maoni na kutoa taarifa yake na ushauri juu ya nini kitekelezwe.

Inavyoonekana, ni dhahiri kwamba wanasiasa na wanaharakati wanajaribu kubeba ajenda ya Katiba Mpya na Tume Huru ya Uchaguzi kama sehemu ya kutoa madukuduku yao bila kujali kwamba masuala hayo yanabeba mustakabali wa taifa kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Ni vyema masuala hayo, hususan Katiba Mpya, yakapata muda wa kuyatafakari kwa kina, mapana na marefu ili kuwa pamoja na kuwashirikisha wananchi ambao ndio wenye umiliki wa katiba na si vyama vya siasa.

Hiyo ina maana kwamba kama ni kuanza upya kwa mchakato na kuachana na Katiba Inayopendekezwa iliyotokana na Bunge Maalum la Katiba ni lazima wananchi washirikishwe juu ya yale yaliyomo ndani yake. Kadhalika, hata kama mchakato utaanza upya, wananchi pamoja na makundi mbalimbali yatashirikishwa katika hatua ya ukusanyaji maoni na hatimaye kuwa na rasimu itakayopita hatua mbalimbali kabla ya kuwa katiba kamili.

Kwa mantiki hiyo, ni vyema kukawa na subira kwa kuwa suala hilo limeonekana kuwa halina kikwazo mahali popote , hivyo kila kundi au wadau wa masuala ya siasa na taifa kwa ujumla ni vyema wakawa na subira kusubiri maandalizi na hatimaye kazi kuanza.


Ni dhahiri kwamba suala hilo lina masilahi kwa taifa na linabeba mustakabali wake, hivyo kunatakiwa utaratibu maalum katika kutekelezwa kwake badala ya kuwapo dhana kwamba makundi fulani ya watu ndiyo yanayotaka jambo hilo lifanyike. Kwa maneno mengine, Katiba ni lazima iwe na sura ya utaifa badala ya kuonekana kama inahodhiwa na watu wa makundi fulani.

Pia ni dhahiri kwamba hata Tume ya Uchaguzi inayodaiwa kuwa ina kasoro mbalimbali ikiwamo dhana kwamba haina uhuru katika kutekeleza majukumu yake, itakuwa rahisi kupatikana ile inayosimamia haki iwapo Katiba Mpya itapatikana.

Kutokana na hali hiyo, ni vyema kukawa na utulivu na maelewano baina ya wadau wote wanaohitaji Katiba Mpya na kisha Tume Huru ya Uchaguzi. Watu wote, ikiwamo serikali, wana lengo jema la kupatikana kwa vitu hivyo katika kuimarisha demokrasia na utawala bora, hivyo hakuna haja ya kugombea fito kwa kuwa nyumba inayojengwa ni moja ambayo ni Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hoja ya kuwa na katiba mpya isigeuzwe mtaji wa wanasiasa

Na Sabato Kasika

**NCHI** kuwa na katiba mpya, ni hoja ambayo inaendelea kutawala katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, huku wadau mbalimbali wakiwamo wanasiasa, wakionyesha shauku ya kutaka ipatikane.

Mjadala wa katiba mpya ndio ambao kwa sasa umeshika baada ya CCM kuiagiza serikali kuangalia jinsi ya kufufua mchakato huo kwa kuzingatia mazingira ya sasa kwa maslahi mapana ya taifa na maendeleo kwa ujumla.

Kwamba, mazingira ya siasa yaliyokuwapo miaka sita iliyopita, chama hicho kilikuwa na msimamo tofauti kutokana na kuweka kando mchakato wa katiba mpya baada ya kumalizika kwa Bunge Maalum la Katiba mwaka 2014.

CCM imekubali kuhuisha mchakato huo, kutokana na maslahi kwa taifa hatua ambayo inaonyesha kuwa sasa imeachana na msimamo wa awali wa miaka kadhaa kuhusu kuwapo katiba hiyo.

Mchakato wa katiba mpya ulikwama mwaka 2014 baada ya kumalizika kwa Bunge Maalum la Katiba, ukiwa katika Katiba Inayopendekezwa ambayo hadi leo inasubiri kupigiwa kura ya maoni.

Hata hivyo, kabla ya bunge hilo kumalizika, ilitokea sintofahamu ambayo ilisababisha baadhi ya wajumbe wake kutoka vyama vya upinzani kulisusia wakidai kuwa limeegemea kwenye matakwa ya vyama si ya wananchi.

Wajumbe kutoka vyama vya upinzani waliosusa bunge hilo, waliungana na kuanzisha Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), ambao ulikuwa na nguvu kubwa, ingawa kwa sasa ni kama haupo tena.

Baada ya kugusia hayo kidogo, sasa ninajielekeza kwa kile ninachotaka kukijadili, ambacho pia kimegusiwa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, hasa hoja ya katiba mpya.

Anataka hoja ya katiba mpya isitekwe na wanasiasa, kwa kuwa katiba mpya si ya wanasiasa bali ni yenye masilahi kwa taifa, na kwamba kila mwananchi anatakiwa kuelimishwa ili atakapoamua awe na uelewa mpana.

Ninaunga mkono kauli hiyo hasa ninapokumbuka yale yaliyotokea kwenye Bunge Maalum la Katiba ambayo yalisababisha baadhi ya wajumbe kususa bunge na kubaki wale ambao karibu wote walikuwa upande mmoja.

Hivyo, wakati huu ambao mjadala wa katiba mpya unaendelea, ingekuwa ni vyema utakapofikia wakati wa kuandaa taratibu za kuifanikisha, basi wanasiasa wasiugeuze kuwa wao, kwani yaliyotokea mwaka 2014 yanajulikana.

Iwapo kutakuwa na haja ya kuwa na Bunge Maalum la Katiba, basi vyema washirikishwe wajumbe ambao hawana mrengo wa chama chochote cha siasa, bali wawe wanaozingatia maslahi mapana ya taifa.

Kwa njia hiyo, ni wazi nchi inaweza kupata katiba ya wananchi na siyo ya wanasiasa ambayo inaweza kuwa imetengenezwa kwa kuzingatia maslahi ya chama badala ya umma, na hivyo kusababisha msuguano.

Siyo kwamba wanasiasa hawana umuhimu kwenye mchakato wa katiba mpya, bali ninachokusudia ni kutaka wasiwe na nguvu kubwa kuliko wadau wengine wasio na vyama, kwani wanaweza kurudisha yaliyotokea 2014.

Badala ya kujadili hoja, baadhi ya wajumbe waliegemea kwenye maslahi ya vyama vyao na hivyo kusababisha mvutano usio wa lazima huku baadhi ya hoja za muhimu zikiwekwa pembeni.

Ikumbukwe kuwa, mchakato wa katiba mpya ulianza mwaka 2011 wakati wa serikali ya awamu ya nne, ambapo tangu wakati huo, CCM imekuwa ikilaumiwa kwamba ilivuruga mchakato huo.

Hivyo, ili lawama za aina hiyo zisijirudie, ni vyema wanasiasa kutoteka hoja ya katiba mpya na kuifanya kuwa yao, badala yake wanaweza kuwa wachombezaji tu, kwa lengo la kuhakikisha inapatikana.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA



Na Pascal Mayalla

Kwa muda mrefu baadhi yetu tumekuwa tukilalamikia baadhi ya sheria ambazo zinawakosesha haki Watanzania zikiwamo zinazohusiana na uendeshaji wa siasa za vyama vingi nchini.

# Rais Samia akitekeleza hili hakika Tanzania itabarikiwa

KILA jambo hutokea kwa sababu, hata likiwa jambo baya. Kunaweza kutokea jambo baya kumbe lina wema ndani yake kama ilivyo mfano wa Yesu kwa Wakristo, alikuja ili kuukomboa ulimwengu.

Yesu Kristo aliteswa hadi kufa msalabani na hili ni jambo jema kwani kwa kupigwa kwake na kwa kuteswa kwake, wanaomwamini walipona. Ukombozi ulipitia mateso na kifo cha msalabani na ile dhambi ilikufa.

Aliyashinda mauti kwa ufufuko na kuwaachia waamini wake milele japo miili ya kidunia itakufa wakati mwili wa kiroho haufi na tukapata uzima wa milele.

Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, alikuwa ni chaguo la Mungu kwa Tanzania. Akayafanya yale aliyoweza kuyafanya, kuchonga barabara na mambo mengi hadi kuitwa Tingatinga.

Magufuli, kama alivyokuwa akijulikana kama JPM, alikuwa mpango wa Mungu kwa Tanzania.

Ujio wa Samia Suluhu Hassan pia ni mpango wa Mungu kwa Tanzania. Mpaka hapa tulipofika, Rais Samia ameishaonyesha kwa kauli na matendo kuwa na yeye ni mpango wa Mungu kwa Tanzania, hivyo Watanzania tunapaswa kusema Asante Mungu kwa Samia.

Tunasema asante Mungu kwa JPM na asante Mungu kwa Samia. Kwa mazuri ambayo Rais Samia sasa anayafanya, tumpongeze kwa mazuri yake bila kumlinganisha na mtangulizi wake.

Mara tu baada ya kuingia, Samia ameruhusu watu kuzungumza na kuikosoa serikali yake lakini kwa staha.

Jambo la msingi analosisitiza ni uzalendo na hata unapokosoa fanya kwa kutanguliza maslahi ya taifa na uzalendo kwa ujumla.

Kwa mantiki hiyo, kukiwa na jambo lolote ambalo si jema, si zuri, si la kupendeza, tuliseme kwa nia ya kulionyeshea na tutoe ushauri wa nini cha kufanya. Ushauri huo si kumpangia bali ni kumshauri tu.

Kwa muda mrefu baadhi yetu tumekuwa tukilalamikia baadhi ya sheria ambazo zinawakosesha haki Watanzania zikiwamo zinazohusiana na uendeshaji wa siasa za vyama vingi nchini.

Ukilalamikia jambo fulani, ukaliangazia, wenye mamlaka wakalisikia, watatoa kauli kuwa jambo hilo litashughulikiwa. Kitu cha kwanza ni kwa wewe uliyelalamika kusema asante, kilio chako kimesikika na kitu cha pili ni kumshukuru huyo aliyesikia kilio chako na kuahidi kushughulikia jambo lako.

Wiki hii Tanzania imeadhimisha miaka 30 ya mfumo wa vyama vingi nchini. Vyama vingi vilipoanza tena nchini Tanzania mwaka 1992 nilikuwa na mwaka mmoja kazini. Nilianza kazi Januari 2, 1990, hivyo mfumo wa vyama vingi ulinikuta kazini.

Mpaka sasa tunatimiza miaka 30 ya vyama vingi nchini, mimi niko 'Newsroom' na kati ya marais sita wa Tanzania, nimepata bahati ya kufanya mahojiano ya ana kwa ana na wanne. Maombi ya kufanya mahojiano na Samia yako njiani.

Katika miaka yangu 30 ya mfumo wa vyama vingi, nimefanya vipindi vingi, nimehoji watu wengi, akiwamo Mama Samia nimefanya nae mahojiano ya saa moja mara mbili, mara ya kwanza akiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais na mara ya pili akiwa Makamu Mwenyekiti Bunge Maalum la Katiba.

Miongoni mwa makubwa ambayo nimekuwa nikilalamikia ni sheria yetu ya uchaguzi na makala zangu mbili zilizotangulia kabla ya hii, nilieleza jinsi sheria hizo batili na kinyume cha katiba, zilivyokuja kuhalalishwa kwa kuchomekewa ndani ya katiba yetu.

Juzi, katika waraka wake wa Miaka 30 ya Vyama Vingi nchini Tanzania, huku kwenye mtandao wa jamii unaoongoza nchini Tanzania, Jamii Forums, kuna makala inayosambaa iliyoandikwa na mwandishi kwa jina la "Ameandika Rais Samia Suluhu Hassan: Miaka 30 ya Vyama Vingi - Changamoto na Mustakabali Kusonga Mbele".

Nanukuu "Nimedhamiria kwamba kwenye kuenzi miaka yetu ya demokrasia ya vyama vingi. Serikali yangu itajitahidi kufanya mabadiliko katika mifumo ya kisiasa, kiuchumi na katika sheria zetu za uchaguzi.

Lengo ni kwamba Tanzania yetu iende na wakati na kama ilivyokuwa wakati mwingine, tujue mapema ni wakati gani wa kufanya jambo, hata kama si watu wanaliunga au hawaliungi mkono kwa wakati husika.

Mabadiliko katika sheria zetu za uchaguzi, yataleta ushindani wa haki na kuwapa watu fursa ya kuwachagua wawatakao kuwaongoza." Mwisho wa kunukuu.

Japo hii ni ahadi tu, hili ni jambo jema kwa sababu tumelipigia sana kelele.

Haki huinua taifa. Kwa ahadi kama hizi, Rais Samia anazidi kuthibitisha yeye ni Chaguo la Mungu kwa Tanzania na akitekeleza haya, atabarikiwa na taifa litabarikiwa.

Asante Mungu kwa Rais Samia, Mungu Ibariki Tanzania.

**Paskali 0754270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

Ukiwa mtaani ukasikia Watanzania wanavyosifia Kiswahili utadhani kweli wanamaanisha na hawapati usingizi kukiwaza na kukienzi. Utasikia Kiswahili kilituunganisha mpaka tukapata uhuru kutoka kwa mkoloni. Basi inaishia hapo.

# Waswahili tusiojua Kiswahili tutakienzi!

WATANZANIA tuna kila sababu ya kujivunia na kuienzi tarehe 7/7 ambayo ilizaa Sabasaba na kihistoria ni siku ambayo mwaka 1954 chama kilichoitwa kwa Kiingereza Tanganyika African National Union (TANU) kilizaliwa.

Mwalimu Julius Nyerere na wenzake walikianzisha wakati huo kupambana na wakoloni ili kuliacha taifa letu la Tanganyika likiwa huru nasi tujiamulie mambo yetu wenyewe.

Na kweli ilipofika Desemba 9, 1961 tukapata uhuru wetu chini ya chama hicho hicho cha TANU ingawa hatimaye kikaungana na Afro-Shiraz Party (ASP) cha Zanzibar na kuzaliwa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Nasema ni siku ya kuienzi kwa sababu pia ni siku ambayo wafanyabiashara nchini hufikia kilele cha maonyesho ya biashara zao kimataifa, katika viwanja vya JK Nyerere Dar es Salaam, pale barabara ya Kilwa.

Lakini kama hiyo haitoshi, ni siku ambayo inatambuliwa duniani kama Siku ya Kiswahili. Mungu atupe nini sasa Watanzania? Tulikipambania Kiswahili mpaka sasa kinatambuliwa na kuheshimiwa duniani. Je, sisi tunakiheshimu?

Ukiwa mtaani ukasikia Watanzania wanavyosifia Kiswahili utadhani kweli wanamaanisha na hawapati usingizi kukiwaza na kukienzi. Utasikia Kiswahili kilituunganisha mpaka tukapata uhuru kutoka kwa mkoloni. Basi inaishia hapo.

Unajiuliza kama kilituunganisha kwa nini leo tunakiacha na kuenzi Kiingereza na malugha mengine ya kighaibuni? Tunafundisha vyuoni kwa Kiingereza, Waswahili wamepiga kelele wee tufundishane kwa Kiswahili.

Aaa Wapi! Mpaka Michael na James wakaigiza angalau kuendeleza kilio, hakuna kitu!

Juzi nikamsikia Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akitoa maelekezo ya jinsi ya kukienzi Kiswahili akitaka sasa kila kitu kiandikwe kwa lugha hiyo kuanzia nyaraka, mikataba, mabango, maelekezo kwenye dawa na majina ya barabara na mitaa.

Kama haitoshi, semina, warsha, mikutano na makongamano yote mambo yawe ya Kiswahili tu na asiyekijua na akae hivyo hivyo, tunaokijua tuserebuke nacho na kukitumia kama mali yetu.

Hii si mara ya kwanza kwa kiongozi wa nchi kufanya hivyo. Alipata kutoa maelekezo hayo Waziri Mkuu wa zamani, Frederick Sumaye, tena akisema kama kwenye mkutano kuna wageni wachache twangeni Kiswahili mtawafasiria. Iko wapi? Iliishia wapi?

Juzi kati hapa akaja Dk John Magufuli (Mungu amhifadhi pema), akahanikiza Kiswahili kila mahali, tukamfuata, wengine kwa nidhamu ya uoga, tukaanza kuhutubia kwa Kiswahili hata palipo Wazungu watupu, yaani tukapitiliza. Alipotangulia, tukaacha!

Yaani sijui tukoje, hivi kwa nini mswahili hataki lugha yake, na ndiyo sababu hata tukishapiga masanga kidogo, tunaanza kubonga Kiingereza, hivi nani alisema usipoongea lugha hiyo basi hujalewa? Au ni lugha ya walevi? Sijui!

Kama kweli tunataka kukienzi Kiswahili na kuonekana vinara wa kukikumbatia kama mali yetu, basi tufanye kweli kama alivyoagiza Dk. Mpango. Tusione mibango ya Kiingereza huko mitaani.

Lakini tutaweza bila hata baadhi ya majina ya makundi yetu au taasisi au kampuni na hata vyama vikiendelea kuitwa majina ya Kiingereza? Mabasi ya sijui nini Trans, nyumba za Guest House, sijui CUF (Civic United Front) haiwezi kuitwa CCW (Chama Cha Wananchi) kama ilivyo CCM (Chama Cha Mapinduzi)?

Kama tutaamua kwa dhati kuwa tunakienzi Kiswahili na kutambua heshima tuliyopewa na Dunia kwa kuwa na Siku ya Kiswahili, bila shaka tutaendelea kusifiwa kama mama wa Kiswahili duniani, lakini tukiendelea hivi hivi. Sijui!

Dk. Mpango akawaambia wanahabari kuwa wajitahidi kutafsiri lugha za kigeni zinapotolewa ili kuhakikisha wananchi wanaowasikiliza au kuwasoma wanaelewa. Tujiulize je, hao wanahabari wetu wanakijua Kiswahili kweli?

Je, vyuo vyetu vya habari vinafundisha Kiswahili kweli kama inavyotakiwa kwa mzungumzaji wa Kiswahili fasaha na sanifu awe? Kama hilo nalo ni gumu, basi tuache kujitapa kwa Kiswahili ambacho hatukijui.

Ukitaka kujua kama hatujui, basi we sikiliza watangazaji tulio nao nchini, uone na kusikia kama wanazungumza kweli Kiswahili kinachotakiwa kuzungumzwa na mtu anayetarajiwa kuwa mwalimu wa Kiswahili ndani na nje ya nchi. Wengi ni Kiswanglish na Kimakonde! Ni Waswahili tusiojua Kiswahili!

**Alamsiki!**



# ULEVI NA UVIVU CHANZO CHA UMASKINI KATIKA FAMILIA

Na Dk. Enock Mlyuka

JAMII yoyote imeundwa na familia. Familia ni serikali ya nyumbani na shule ya kwanza ya mafunzo kwa watoto ambamo raia wema, waumini, viongozi, watumishi, waume na wake bora hutengenezwa.

Familia ni moyo wa shughuli zote (the heart of all activities). Baba na mama ni viongozi wa familia.

Familia inahitaji uongozi, ukaribu na uangalizi wa baba na mama ili maendeleo na ustawi viwepo.

Baba na mama katika familia wasipotimiza wajibu wao ipasavyo wanaweza kuwa chanzo cha udumavu na umaskini katika familia.

Wazazi walevi na wavivu huchangia sana kuleta umaskini katika familia zao.

Umaskini katika makala hii una maana ya hali duni ya maisha na kipato inayosababisha familia kushindwa kukidhi mahitaji ya msingi ya kila siku kama chakula, malazi, mavazi na elimu.

Mungu alipomuumba mwanadamu hakukusudia awe maskini, bali awe na maisha bora. Umaskini uliopo katika familia na jamii umetengenezwa na wanadamu wenyewe kwa sababu ya matendo yasiyofaa.

Tabia ya ulevi wa pombe na uvivu vilivyokithiri miongoni mwa watu kwa sehemu kubwa vimekuwa chanzo cha umaskini katika familia nyingi.

Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya binafsi wa mwaka 2017-2018 uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, asilimia 26.4 ya watu wa Tanzania Bara wana umaskini wa mahitaji ya msingi.

Umaskini wa mahitaji ya msingi ni mkubwa vijijini kwa asilimia 31.3 kuliko mijini ambao ni asilimia 15.8. Vile vile, asilimia nane ya watu Tanzania Bara wanaishi katika umaskini wa chakula.

Kwa ujumla, utafiti umeonyesha kuwa asilimia 81 ya watu wenye umaskini wa mahitaji ya msingi wanaishi maeneo ya vijijini, wakati asilimia 16 wanaishi maeneo ya mijini na asilimia tatu wanaishi katika mkoa wa Dar es Salaam.

### ULEVI NA ATHARI KATIKA FAMILIA

Ulevi wa pombe unachangia umaskini katika familia na kusababisha familia nyingi kukosa utulivu, amani, furaha na maendeleo sawia. Kwa baadhi ya wanandoa, pato la familia kwa sehemu kubwa hutumika katika pombe au kileo kuliko kufanya mambo ya maendeleo. Hali hii husababisha familia kuwa na kipato duni kwa ajili ya mahitaji ya msingi ya kila siku.

Katika maeneo mengi ya vijijini, baadhi ya wanaume hujishughulisha zaidi na ulevi wa pombe kuliko shughuli za maendeleo na uzalishaji. Kazi nyingi za maendeleo na uzalishaji hufanywa na wanawake. Imetokea katika baadhi ya familia wanaume kudai kwa nguvu kipato kidogo kilichotafutwa na wake zao kwa ajili ya kununulia pombe.

Hali hii huihujumu familia kimaendeleo na kiuchumi.

Ulevi wa pombe huathiri afya ya watumiaji hali inayowafanya kuwa mzigo kwa familia zao. Mlevi hawezi kufanya kazi yake inavyotakiwa ili kuiletea familia yake kipato kutokana na udhaifu wa afya.

Utendaji wa kazi wa wafanyakazi walio walevi huwa chini ya kiwango, hivyo kuathiri uzalishaji.

Familia zingine zimejikuta kipato kidogo kinachopatikana kinatumika kwa matibabu ya maradhi yatokanayo na ulevi.

Kwa baadhi ya wanandoa, ulevi umezalisha michepuko mingi kwa kuwa pombe huamsha tamaa ya mwili.

Kwa kutambua hilo, makahaba wengi ambao husaka watu wa kutuliza tamaa zao za mwili au kujipatia kipato, hupenda kukaa maeneo yanayouzwa pombe.

Wanawake hawa wanajua jinsi ya kuwanasa wanaume wanaoonekana wana fedha na walio walewa pombe.

Baadhi ya kina baba hujikuta wakitekwa ufahamu na wanawake wa nje kiasi cha kusahau majukumu katika familia zao. Mara nyingi imetokea penzi la nje linagharamiwa zaidi kuliko familia.

Matumizi ya familia huongezeka kwa sababu ya kutunzwa kwa penzi la nje na watoto wanaotokana na penzi hilo. Gharama za matunzo hayo husababisha maisha duni na manyanyaso katika familia nyingi.

Ulevi huchochea ugomvi na vitendo vya ukatili katika familia. Watu wengi wakilewa pombe akili zao huvurugwa kwa sababu kileo huathiri ubongo.

Wako baadhi ya wanandoa walevi wakitaka kuleta ugomvi nyumbani, huenda kwanza kupata kileo ili kutoa nishai. Hujificha chini ya kivuli cha ulevi kwa kukosa ujasiri wa kusema au kutenda jambo kabla ya kunywa kileo.

Walevi wengine wanaporudi nyumbani huwa kero kubwa na hukosa ustaarabu na heshima. Watoto wa familia za namna hii humwona baba au mama yao ni adui badala ya kuwa rafiki kwa sababu ya matendo ya ukatili anayofanya katika familia anapokuwa amelewa pombe.

Familia nyingi zimesambaratika kutokana na ugomvi wa mara kwa mara unaotokana na pombe. Ugomvi unapotokea kati ya mume na mke, wanaoathirika zaidi ni watoto.

Watoto wanakosa haki ya kufurahia maisha ya wazazi wao. Watoto wanachokishughudia zaidi nyumbani ni ugomvi, vichapo, kuumizana na mauaji kuliko matendo ya upendo kutoka kwa baba na mama.

Matendo ya jinsi hii hutengeneza kizazi cha watu wakatili katika familia na jamii kwani katika makuzi yao ndicho watoto walichokiona na kujifunza kutoka kwa wazazi wao.

Ulevi huathiri afya ya mwili na akili ya mwanandoa. Baadhi ya watu wamepata magonjwa ya afya ya akili, magonjwa ya moyo na kuambukiza; kiharusi, utapiamlo, kupoteza uhai na nguvu za kiume (kinababa) kwa sababu ya ulevi wa pombe.

Ni hakika kwamba, afya ya mtu ikiwa dhaifu huchangia sana kupunguza ufanisi katika utendaji wa kazi ikiwa ni pamoja na tendo la ndoa.

Afya bora ni baraka na mtaji kutoka kwa Mungu. Kwa mantiki hii, afya ya mtu yeyote inahitaji kutunzwa. Mambo tunayopanga kufanya katika maisha yetu hutegemea sana utimamu wa afya zetu ili yafanyike vizuri na kwa ufanisi.

### UVIVU NA ATHARI ZAKE

Uvivu ni adui mkubwa wa maendeleo na chanzo kingine cha ugomvi katika familia nyingi. Baadhi ya wanandoa hawawajibiki katika ndoa zao, bali hupenda kufanyiwa kila kitu na watu wengine.

Baadhi ya familia zimekuwa maskini kwa sababu mmoja wa wanandoa au wanandoa wote wawili ni wavivu.

Hali hii ya kutokuwajibika kwa wanandoa imechangia umaskini na kuleta majaribu katika familia nyingi. Ni dhahiri kwamba maisha mazuri yanahitaji kujituma na kuwajibika.

Kufanya kazi kwa bidii na maarifa ni mpango wa Mungu kwa mwanadamu.

Kwa mantiki hiyo, uvivu ni chukizo kwa Mungu pamoja na jamii.

Mwanandoa asiyewajibika hupunguza umuhimu na thamani yake katika familia yake. Mafanikio hayaletwi kwenye sahani, hivyo, wanandoa wanapaswa kuwajibika katika familia zao kwani mtu anapopambana na uvivu anatatua matatizo mengi.

Mume na mke wanahitaji kusaidiana na kushirikiana vyema katika kutunza mahitaji ya familia ili kujiletea maendeleo. Pamoja kwamba kutunza familia ni jukumu la msingi la baba, mke anayejitambua na mwenye upendo hawezi kumwacha mume wake ahangaike peke yake kutafuta mahitaji ya familia.

Mahali pengine imetokea mke anakuwa na uwezo wa kipato kuliko mume wake. Kwa hiyo, mama anapotumia mapato yake kwa faida ya familia huijenga familia yake kwani mwanamke yeyote ni nguzo ya familia.

Kinababa watambue na kuthamini mchango wa wake zao katika familia ili kuleta hamasa ya kufanya vizuri zaidi badala ya kuwakatisha tamaa.

### HITIMISHO

Ndoa na familia si taasisi za ubabe. Uhusiano baina ya mume na mke si wa kiutawala, kutesana na kufanyiana vitendo vya ukatili, bali ni upendo, staha, kuheshimiana kuwajibika na kufurahishana.

Katika familia tunajifunza namna ya kupendana kadiri tunavyopendwa na kuheshimiwa. Ni katika familia, utamaduni sawia na murua wa huruma, upendo, amani, mshikamano, kuheshimiana, kuhudumiana, kusaidiana, kujaliana, kusameheana, mapato na maridhiano maridhawa hujengwa.

Pia katika familia jamii inajifunza roho ya uwajibikaji, ushirikishwaji, kujali, kuthamini, kulinda na kutunza uhai. Kwa hiyo, baba na mama wapo ili kujenga familia bora na si kubomoa na kuleta umaskini katika familia.

**■Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online.**

**Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

JULAI 10, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana


Ukurasa 15




## Zijue faida na hasara za matumizi ya kitanda cha chuma nyumbani



Ukurasa 13

## MAVAZI YA USIKU YANAYOLEWESHA




## KATUNIKA

Ukurasa 16





# ONDOA VIPELE

## Baada ya kunyoa ndevu

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | P | E | N | D | O |
| ■ | A | ■ | ■ | A | ■ |
| U | G | A | ■ | N | ■ |
| ■ | A | ■ | U | D | A |
| ■ | W | ■ | ■ | I | ■ |
| S | A | N | D | A | ■ |

## AMSHA AKILI

CHORA MSHALE KUONESHA KUVULI HALISI CHA KISHADA HIKI




## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UDA, UMA, SANDA, TAMKO, KANDIA, TAMBUA

## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya Adaktari

MTOTO Grace alikuwa na babu yake wakitembea kwenda shambani. Babu yake alikuwa akitembea taratibu huku akishikilia fimbo, huku Grace akiwa mbele yake akitembea haraka.

Grace alimuuliza babu yake kwa nini anatembea taratibu na yeye anakwenda haraka?

Babu: Mimi ni mzee nguvu zimeniishia lazima nitembee taratibu na wewe ni mtoto una nguvu za kutembea

Grace: Lakini mwalimu alituambia kuwa taratibu ndio mwendo, kwa hiyo sisi tunaotembea haraka tutapata madhara?

Babu: Mjukuu wangu huo ni msemo tu unamaanisha kufanya kitu kwa taratibu unakuwa makini nacho na utakifanya kwa ubora na sio vingine.

SWALI
Kitunguu maji kina faida gani kwa binadamu?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Umeolewa kumbe mchumba wa kwanza bado anakuhitaji

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na simulizi ya kijana mmoja aitwaye Pazi. Alimuoa binti mrembo aitwaye Halima lakini yaliyomkuta alibaki anashangaa. Kumbe vilikuwapo vyanzo ambavyo alivigundua baadaye baada ya kujitosa katika ndoa.

Wiki iliyopita, tuliona mchakato wake wa ndoa ulivyofanyika vyema na kuanza maisha ya mke na mume. Ndani ya miezi sita ikawa bado bibie hajapata ujauzito, yakaanza maswali ya hapa na pale.

Lakini katika kudadisi kwa wanaoitwa “wataalamu”, ikaonekana kuwa yuko kijana mwingine aliyempenda bibie kijijini kwao kabla ya Pazi lakini akakataliwa na kwamba alikuwa anamtafuta ajue anakaa wapi. Halima alipoulizwa kuhusu jambo hilo akakiri ni kweli ilitokea hivyo.

Kijana Pazi wakati anaoa, alikuwa anafanya kazi katika kiwanda cha mablanketi kilichokuwa Dar barabara ya Migeyo. Kiwanda kikaanza kulegalega kiuzalishaji. Siku moja wazungu walitembelea hapo kiwandani na walipokuwa kwenye mzunguko mle kiwandani wakakutana na Pazi akawasalimia, Good morning, wakamjibu morning.

Walipomaliza ziara kiwandani, wazungu wakarudi kwa yule kijana aliyewasalimia kimombo. Mkalimani wao akamuuliza Pazi, unaongea Kiingereza? Mkalimani akarudisha jibu kwa wazungu. Ndipo wazungu wakataka kijana aelezee maisha yake kwa ufupi kwa Kiingereza.

Yule kijana akaulizwa kama yuko tayari kwenda kusomea mambo ya hoteli. Akajibu ndiyo. Basi tutakupeleka chuo cha Forodhani. Akashukuru. Wakamwelekeza mahali atakapowakuta pale Hoteli ya New Africa, akapewa majina mmoja anaitwa Les Sculton na mwingine Maike Smith.

Jumapili akaenda akawakuta Posho Bar, wakasalimiana na kwenda Forodhani. Wakalipa gharama zote na mafunzo na zingine. Wakarudi hotelini na wakampa Sh. 600 na kuagana.

Kule kiwandani wakati anafanya michakato yote hiyo aliaga kuwa mama yake anaumwa hivyo alihitajika kuungana na nduguze kumpeleka hospitalini akaruhusiwa.

Kesho yake akaamka mapema tofauti na kipindi yuko kiwandani, hata koti la kiwanda hajavaa. Huko nyuma wanaulizana mbona leo mzee hajavaa majampa ya kazini? Hakuna aliyejua.

Kijana akafika chuoni akaanza masomo ya uongozi wa hoteli. Siku zinavyozidi pale nyumbani hawamuelewi na kila akirudi hakosi kuja na vichwa vya nguru. Mara siku nyingine vipande vya kuku na hata mwonekano wake ni tofauti na wakati akiwa kiwandani.

Alianza kutakata, kunenepa na baada ya miezi mitatu akapata mapumziko ya siku sita. Akaenda kiwandani kuomba aongezewe mwezi mmoja au aandike barua ya kuacha kazi.

Swali likawa, je, akikubaliwa kuandika barua ya kuacha kazi na kulipwa haki zake zote na akimaliza masomo Forodhani atapata bahati ya kuajiriwa?

Kijana akaambiwa aandike barua ya kuacha kazi, jambo ambalo alitekeleza na kulipwa mafao yake yote. Akawa anaendelea na masomo kule Forodhani. Baadaye akapangiwa kwenda Ngorongoro kufanya mafunzo kivitendo (field) miezi mitatu.

Alipomaliza akaajiriwa New Africa Hotel na baada ya miezi sita akahamishiwa Mikumi Lodge. Kufikia hapo, yule kijana ikabidi amweleze mkewe kazi anayofanya. Akamwambia kwa sasa amehamishiwa Mikumi Lodge. Bibie akagoma kwenda Mikumi akadai amrudishe kwao. Huyu kijana alikuwa mpenzi sana wa sinema.

Kijana hakuelewa kinachoendelea. Kumbe, kijana aliyekataliwa kumuoa binti kijijini ndiye anayemvuruga akatae kwenda Mikumi arudishwe kwao na atoe talaka, kisha apate nafasi ya kumuoa binti.

Mipango hii yote ya kijana yule wa kijijini, bibie wala mumewe hawajui.

Wakafunga safari ya kwenda kijijini na kupokewa. Kesho yake binti akawaeleza wazazi wake kwamba amerudi lakini pia anataka apewe talaka. Baba akamwuliza sababu za kudai talaka, akajibu, “nimeamua tu”.

Familia zote mbili zikakutana kuliweka sawa lakini binti akagoma. Basi kijana naye akagoma kutoa talaka na abaki.

Akiwa pale kijijini, kumbe bibie anawasiliana na kijana aliyemkataa. Kijana akamtuma mshenga kuja kwa baba yake Halima. Mzee akamfukuza na barua aliyoleta akaichoma moto. Kumbe siku chache huyo kijana tayari wana uhusiano na bibie na tayari ni mjamzito.

Kijana akaleta Sh. 50,000/= mzee akauliza pesa ya nini? Akamwambia soma barua utaelewa tu, kumbe ni barua ya uchumba. Mzee hakuendelea kuisoma ile barua akamrudishie ile pesa na barua akaichoma moto!

***Mpenzi msomaji, kwa leo niishie hapa. Wiki ijayo tutaona jinsi mke wa Pazi alivyotibua ndoa yao kwa kubeba ujauzito wa mchumba aliyemkataa kwanza kule kijijini kwao. Je, una maoni, kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Sensa ni kwa faida yetu tujitokeze kuhesabiwa

SENSA ya Watu na Makazi hufanyika kila baada ya miaka 10 kwa ajili ya nchi kutambua idadi ya watu wake, umri wao, kazi na shughuli za uzalishaji wanazofanya kwa lengo la kuiwezesha kupanga maendeleo vizuri.

Hii ni sensa ya sita kufanyika baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964. Sensa zingine zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012.

Kwa sasa, serikali imebainisha kuwa maandalizi ya sensa ya Agosti 23, mwaka huu, yamefikia asilimia 87 na kwamba kila kitu kinakwenda vizuri kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na kuhesabiwa.

Sensa ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathimini, kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), sensa ni suala maalum lenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, kwa umri na jinsi, mahali wanapoishi na hali zao za elimu, hali ya ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makazi.

Aidha, takwimu hizo za msingi ndizo zinazoweza kuainisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwamo makundi maalum yenye uhitaji kwa mfano watu wenye ulemavu, wanawake, watoto, vijana na wazee, hivyo kurahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na uhitaji na mazingira yaliyopo.

NBS inasema umuhimu wa kipekee wa sensa kwa mwaka huu ni kuisaidia serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, mageuzi ya masuala ya afya na jamii pamoja na ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa.

Sensa pia husaidia mamlaka za serikali za mitaa katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu katika ngazi husika na kusaidia kwenye uwiano wa mgawanyo wa rasilimali.

Aidha, husaidia kupata taarifa za hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi za idadi ya watu na makazi na mipango katika ngazi zote.

Pia kigawio katika kukokotoa viashiria vingine mfano pato la mtu mmoja mmoja, pato la taifa, ajira na ukosefu wa ajira na kiwango cha uandikishaji wanafunzi.

Aidha, taarifa itawezesha serikali kujua ongezeko la idadi ya watu, kwa mgawanyo na viashiria vingine, ambavyo ni muhimu kwa usimamizi wa mazingira.

Pia msingi wa utawala bora na ujumuishaji wa demokrasia, kwa kuwa takwimu sahihi za sensa zinahitajika kwa ajili ya ugawaji wa majimbo ya uchaguzi kwa ufanisi, kurekebisha mipaka ya kiutawala katika serikali za mitaa.

Ili sensa ifanyike ni lazima kuwe na uwekezaji wa fedha kuanzia maandalizi hadi siku yenyewe kwa kuwa watu wataajiriwa kwa muda na watalipwa fedha kwa ajili ya kazi hiyo.

Hizi ni fedha za Watanzania, yaani zetu sote, hivyo tunapaswa kushiriki ili zitumike kwa uhalali na kuleta matokeo tarajiwa kwa manufaa yetu sote.

Sensa ya mwisho ilionyesha kuna takribani Watanzania milioni 43.6 na sasa inakadiriwa kuna zaidi ya watu milioni 56. Kupitia sensa ya mwaka huu, zitapatikana takwimu sahihi tofauti na zile inazotolewa kwa makadirio ya ongezeko la watu kwa asilimia kwa mwaka kulingana na eneo husika.

Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kila Mtanzania akashiriki kuhesabiwa na kuhamasisha wengine kutoa ushirikiano kwa makarani watakaofanya kazi hiyo kwenye maeneo yao.

Ni vyema watu hususan wa maeneo ya vijijini na pembezo kutambua umuhimu wa sensa, kuacha imani tofauti ambazo si sahihi hasa katika kuhesabu watu kwa kuwa hakuna ukweli wowote katika kila wanachoamini .

Kutoshiriki sensa ni kutoshiriki mchakato wa maendeleo yako binafsi na taifa kwa ujumla. Pia ni kukwamisha au kuifanya serikali isipate taarifa sahihi za idadi ya watu wake ili inapopanga mipango iwajumuishe kwa ukamilifu wake.

Ni sawa na ndani ya familia baba au mama hununua mlo kulingana na idadi ya wanafamilia. Anapoongezeka mwingine maana yake hakuwa kwenye hesabu, hivyo itakuwa vigumu mlo ulioandaliwa kutosheleza kwa sababu waliopo watapunjika.

***Mungu ibariki Tanzania***





Ilikuwa shangwe, vifijo na nderemo baada ya Willson Kitaa kufunga pingu za maisha na Nazahedi Kisaka, katika Kanisa la Waadventista Wasabato Mbezi Luis jijini Dar es Salaam Juni 26 mwaka huu na kufuatiwa na sherehe iliyofanyika Mbezi.Tunawatakia maisha mema ya ndoa.










## MITINDO

# MAVAZI YA USIKU YANAYOLEWESHA

ILI kuwa na utulivu chumbani, mwanamke anatakiwa kuwa mbunifu kwa aina ya mavazi yake ya kulalia akiwa na mwenza wake.

Kuvaa aina tofauti ya nguo nyakati za usiku humfanya mwanaume kuhisi yupo salama na mwenye umakini zaidi.

Kuna aina nyingi ya nguo ambazo zinavaliwa usiku, lakini kwenye safu hii, itaelezwa baadhi ambazo mwanamke akivaa husababisha mahaba kuongezeka.

**FULANA KUBWA**

Ni vazi la kawaida, lakini likivaliwa usiku chumbani linamfanya mwanamke kuonekana kuwa mdogo, hivyo humfanya mwanaume kuhisi amefanya chaguo zuri.

**SHATI LAINI**

Shati laini lisilobana mwili ni vazi zuri kuvaliwa usiku. Unachotakiwa hakikisha sehemu ya juu hufungi vifungo na hivyo shingo na mabega huonekana vizuri.

**PAJAMA FUPI**

Ni wazi vazi hili limebuniwa kwa ajili ya kulalia, lakini unaweza kuvaa wakati ukifanya mazungumzo na mwenza wako.

**HAKUNA MAANDISHI**

Hakikisha nguo unazotumia usiku zisiwe na maandishi kwani maneno mengine yataleta kero.







UREMBO

Na Mary Geofrey

# ONDOA VIPELE
## Baada ya kunyoa ndevu



KUTOKWA na upele baada ya kunyoa ndevu ni tatizo linalodharauliwa, lakini wakati mwingine husababisha maumivu ambayo huwa hatari yakiendelea.

Ni vizuri kuepuka hali hiyo kwa kuchukua tahadhari, kama kutotumia wembe wa zamani au uliochakaa na kujitibu wewe mwenyewe pale inapotokea.

Sio wote wanapata vipele na rangi nyeusi, ila kwa wale wenye hali hiyo inachangiwa na vitu vifuatavyo

Kunyoa bila kulainisha ngozi, kupaka spiriti au 'aftershave' yenye kilevi baada ya kunyoa.

Sababu nyingine ni kutokupaka kitu chochote baada ya kunyoa, kutumia wembe usio na makali.

Ufanye nini ili usipate vipele na uondoe weusi?

Ni muhimu kulainisha ngozi yako kabla ya kunyoa. Sehemu ya juu ya ngozi ina chembe hai zilizokufa, ukilainisha kabla ya kunyoa itasaidia kuondoa. Pia itasaidia wembe kuteleza vizuri kwenye ngozi bila kusababisha michubuko.

Utakiwa kutumia aftershave ili kupooza ngozi, kuipa unyevu nyevu na kufanya kuwa nyororo. Spiriti na aftershave zenye kilevi zinafanya ngozi kuwa kavu, itasababisha miwasho na ukijikuna ndo inapelekea kutoka vipele.

Nyoa kufuatisha muelekeo wa nywele zilivyoota.

Hii itasaidia ngozi isiume zaidi wakati wa kunyoa. Pia hakikisha kiwembe unachotumia ni kikali, kikiwa butu utarudia mara nyingi na kuumiza ngozi.

Usitumie 'deodoranti' yenye chumvi ya aluminum na kilevi.

Chumvi ya aluminum na alcohol inachangia kufanya ngozi iwe kavu na kuwasha baada ya kunyoa ambayo itapelekea kupata weusi wa kwapa.

Maji ya uvuguvugu ya chumvi husaidia kama mapele yataendelea na tatizo likiongezeka muone daktari.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Tengeneza 'Popcorn' nyumbani

BISI au maarufu kama 'POPCORN' ni chakula kizuri kama kichangamsha kinywa ambacho hutengenezwa kwa kutumia mahindi.

Mahindi haya hukaangwa na kupasuka ndipo hubadilika na kuwa bisi.

Watu wengi wamezoea kula bisi za kununua kwa sababu hawafahamu namna ya kuzitengeneza.

Leo tutajifunza namna ya kuzitengeneza wenyewe nyumbani tena kwa kutumia njia rahisi ya asili.

**Mahitaji**

Mahindi ya bisi kiasi, mafuta, sukari na Iriki robo kijiko.

**Jinsi ya kutengeneza**

Chukua sufuria weka jikoni tia mafuta yakipata moto kidogo tia mahindi ya bisi na kisha koroga mpaka yakianza kupasuka funika sufuria.

Hakikisha kila mara unayageuza geuza kwa kupepeta sufuria mpaka yote yapasuke.

Yakishapasuka toa weka pembeni, chukua sufuria lingine tia sukari kiasi unachopenda na iriki na ibandike jikoni mpaka sukari ikianza kuyeyuka tia bisi zako.

Anza kuzikoroga polepole zote ziingie sukari vizuri baada ya hapo ipua ili ipoe.

Zikisha poa furahia bisi zako kwa kula moja moja.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Zijue faida na hasara za matumizi ya kitanda cha chuma nyumbani

MOJA ya vitu muhimu ambavyo mtu hununua katika nyumba yake ni kitanda. Hii ni kutokana na umuhimu wake hasa kwa kupumzisha mwili baada ya shughuli za kutwa nzima.

Kitanda cha chuma nacho kinapowekwa kwenye chumba nyumbani, kina mvuto wake kwenye nyumba.

Mbali na kuleta mvuto kwenye chumba, Peter Sinkome ambaye ni mtengenezaji wa vitanda vya chuma katika eneo la Bunju A, anaeleza faida na hasara za kutumia aina hiyo ya kitanda.

Kwa upande wa faida, anasema kitanda cha chuma ni imara na kina uwezo wa kudumu kwa muda mrefu.

Faida nyingine anasema kina uwezo wa kuhimili uchakavu na hakiharibiki kirahisi hata pale kinapokuwa kimetengenezwa kwa mtindo wa kubebana, juu na chini, maarufu kama deka.

Nyingine, anasema kitanda hicho ni chepesi kulinganisha na kitanda cha mbao ngumu na kwamba ni rahisi kukipangilia kwenye chumba namna unavyotaka.

Hata unapotaka kukifungua kwa ajili ya kukisafisha kwa ndani zaidi au kwa kuhamisha katika chumba kingine, hakisumbui kwa sababu ni rahisi kukifungua.


Pia anasema kitanda cha chuma kina matumizi madogo ya eneo la chumba kwenye nyumba kwa sababu miguu yake ni myembamba tofauti na ilivyo kwa kitanda cha mbao.

Sambamba na hilo, anasema kwa kawaida kitanda cha chuma kimepanda juu, hivyo kinampa msafishaji urahisi wa kufanya usafi hadi chini ya uvungu.

Kuhusu hasara zinazotokana na kitanda hicho kwenye nyumba, Sinkome anasema ni kuharibika kwa mipira inayokuwa imewekwa kwenye miguu inayokishikilia ambayo inaposagika na isipobadilishwa kwa haraka huharibu sakafu hasa pale kinaposogezwa.

Na kwamba kitanda hicho kina kawaida ya kubadilika kuendana na hali ya joto au baridi endapo chumba kikipata baridi au joto, huwa vivyo hivyo kwa kitanda kuwa na joto au baridi katika nyakati za baridi na pia kitanda hicho hushika kutu.

"Kitanda cha chuma kinaweza kisiwafae watu wa mabondeni ambao nyumba zao zinatuama maji sakafuni kwa sababu, endapo maji yakituama kwenye chumba kwa zaidi ya siku tatu upo uwezekano mkubwa wa kutoboa sakafu na kudumbukia ndani kidogo kidogo lakini pia miguu ya kitanda chake inaweza kuharibiwa na kutu," anasema Sinkome.



## Namna ya kuchagua redio ndogo ya kidijitali




WATU wengi hawapendi sana kutumia redio ndogo za dijitali ndani ya nyumba, lakini chombo hicho kina umuhimu katika maisha ya kila siku.


Redio za dijitali hazipokea tu vituo vya kawaida vya VHF, pia zinatoa nafasi kwa vituo anuwai ambavyo vinaweza pia kupatikana kitaifa.

Uteuzi wa redio ya aina hiyo inavutia na ubora wake wa usafirishaji upo juu kuliko zile za kawaida.

Zifuatazo ni njia rahisi za namna ya kuchagua redio ndogo za kidijitali.

1: Angalia kama vitufe vya kubonyeza kutafuta chaneli au masafa vipo vizuri.
2: Angalia sehemu ya kuchomeka waya wa kuchaji betri kama ipo vizuri, hakikisha kwa kuweka waya na usikilize vyema.
3: Hakikisha kama spika inafanya kazi kwa ubora unaotakiwa.
4: Angalia kama ina sehemu ya kuweka chipu, flashi na spika ya ziada kama zipo.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
OFA ZA SIKUKUU WATU WANAAGIZA BIA KAMA WANAWAZIMU! SITAKI KUTOLEWA BAR NA MACHELA IKAWA WIMBO MAJUKWAA YA SIASA!
BAR
WOOOH! YWIIIII... UKIWA GANI HUU SIKUKUU SINING'INII KAUNTA KISA DOZ!
LEO NI SIKUKUU YA KUALIKANA, LAKINI SURA ZINGINE KUPATA MUALIKO KIPENGELE!
AAAH! UNAJIONA PISI KALI AU SIO?
DERAVA TUMWAGE BABAAAAA...
ATUSHUSHE AKUMWAGE
KESHAKULA MIPILAU YAKE IMEMLEVYA ANAROPOKA
JAMANI TUSALI BREKI SIZIONI
WE KELELE WEWE
NA WEWE DEREVA USITULETEE WAZIMU KAMA UMEKULA PILAU LENYE VIUNGO VYA BANGE
YAANI HATA UKISEMA NIKUBEBE KICHWANI
ILIMRADI NIMSAHAU ULIYENI-FUMANIA NAE
SIKUKUU IME-BANDANA NA WIKIENDI LEO TWAFA!
TUZIBANDUE BHANA ZIWE 'TAFAUTI' AU SIO MSELA?
LELA KUKUTANIA KUWA NAKUPENDA UMEKUWA SIRIAZ?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...KUYUMBA NA KUANGUKA KWA MLEVI NDIO STAREHE YAKE

## Russia yazidi kushambulia Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

WANAJESHI wa Russia wameendelea kuchanja mbuga katika eneo la mashariki mwa Ukraine la Donetsk, huku Marekani ikiahidi msaada mpya wa kijeshi na mtambo wenye nguvu wa kurusha roketi.

Baada ya kustahimili mapigano ya kipindi kirefu na kuidhibiti miji kadhaa katika eneo jirani la Luhansk, Russia sasa ipo katika juhudi za kuingia zaidi mjini Donetsk ili kuunganisha eneo lote la Donbas.

Duru zilieleza kuwa mitetemo ya mashambulizi ya angani imesikika usiku kucha wa kuamkia jana katika upande wa mashariki na kusini mwa Ukraine.

Wakazi katika mji mdogo wa Druzhkivka uliopo upande wa mji wa kiviwanda wa Kramatorsk waliamshwa na kile kinachodhaniwa shambulizi la kombora lililovuruga duka moja kubwa la bidhaa.

Kadhalika kupitia ukurasa wake wa telegram, mkuu wa utawala wa kijeshi katika eneo la Donetsk, Pavlo Kyrylenko ameituhumu Russia kwa kuyashambulia mashamba na kujaribu kufanya maangamizi katika kazi ya mavuno.

**DW**

## Kinyang'anyiro cha kumrithi Waziri Mkuu wa Uingereza: Ni yapi mapya?

WAZIRI wa zamani wa Usawa nchini Uingereza, Kemi Badenoch amekuwa mwanachama wa nne chama cha Conservative kutaka kuwania kiti cha uwaziri mkuu baada ya Boris Johnson kujiuzulu.

Zimekuwa ni siku chache za heka heka katika siasa za Uingereza tangu tangazo la kujiuzulu kwa Boris Johnson siku ya Alhamisi.

Wabunge hao wanajitokeza katika mapambano ya kuwa kiongozi wa chama hicho na kuwa Waziri mkuu

Kemi Badenoch ambaye ana asili ya Kiafrika amekuwa mbunge wa hivi karibuni wa Conservative kuingia katika kinyang'anyiro hicho

Rishi Sunak alitangaza azma yake siku ya Ijumaa kuwania nafasi hiyo pamoja na kuanzisha kampeni yake rasmi aliyoiita 'Ready for Rish'.

Aidha, Tom Tugendhat, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje na Mwanasheria Mkuu Suella Braverman pia wamewasilisha majina yao kuwania kiti hicho

Mwanakampeni ya Brexit Steve Baker alisema ataunga mkono azma ya mwanasheria mkuu Suella Braverman ya kuwania kiti hicho

Wengine wanaotajwa kuwa wanaangalia uwezekano wa kuwania wadhifa wa Boris Johnson ni Waziri wa zamani wa Afya Sajid Javid, Waziri wa Ulinzi Ben Wallace na Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje, Jeremy Hunt

Muda uliopangwa kwa ajili ya uchaguzi wakiongozi wa chama cha Conservative unatarajiwa kuthibitishwa wiki ijayo na Waziri mkuu mpya anatarajiwa kuchukua wadhifa huo mwezi Septemba.

**BBC**

# Raia waiteka Ikulu Sri Lanka, rais akimbilia sehemu salama

**COLOMBO,** SRI LANKA

RAIS wa Sri Lanka Gotabaya Rajapaksa, anaripotiwa kuikimbia Ikulu baada ya waandamanaji kuivamia na kuiteka.

Hata hivyo, maofisa wa polisi walisema kiongozi huyo alipelekwa mahali salama baada ya makundi ya watu kuvunja kizuizi kilichokuwa kimewekwa nje ya kasri la rais.

Sri Lanka inakabiliwa na mzozo mbaya zaidi wa kiuchumi tangu ipate uhuru huku kukiwa na uhaba mkubwa wa mafuta na dawa.

Maelfu ya waandamanaji wanaomtaka Rais Rajapaksa na serikali yake wajiuzulu,walivamia makazi yake jana.

Akizungumza na shirika la habari la dpa, Ofisa mmoja mwandamizi wa ulinzi alisema rais huyo alisindikizwa na kupelekwa mahali salama.

Maandamano katika makao ya kiongozi huyo yamekuwa yakifanyika mara kwa mara katika wiki za hivi karibuni, lakini hawakuweza kuingia ndani ya jengo la rais.

Maofisa wa usalama walifyatua risasi hewani ili kujaribu kuwazuia waandamanaji, lakini walizidiwa nguvu na kuiteka Ikulu.

Waziri Mkuu aita mkutano wa dharura

Kutokana na sintofahamu hiyo, Waziri Mkuu Ranil Wickremesinghe, aliitisha mkutano wa dharura wa wakuu wa vyama vya kisiasa.

Alitoa wito kwa spika pia kuita kikao cha bunge cha dharura, ilisema taarifa kutoka ofisi ya waziri mkuu.

Wickremesinghe awali aliwahi kueleza nia yake ya kutaka kuunda serikali ya kitaifa kwa kuvishirikisha vyama vyote vya kisiasa.

Kisiwa cha Sri Lanka kinakabiliwa na mzozo mbaya zaidi wa kiuchumi tangu kilipopata uhuru mwaka 1948.

Rais anapinga wito wa kujiuzulu, lakini katika hatua ya kutaka kuwaridhisha waandamanaji, amewaachisha kazi jamaa zake kadhaa waliokuwa wanashikilia nyadhfa za juu serikalini, wakiwemo ndugu zake wawili waliokuwa wanahudumu kama waziri mkuu na waziri wa fedha.

Waziri mkuu kwa sasa yeye ndiye anayeiongoza wizara ya fedha.

Ameahidi kuanzisha mpango wa kuwaletea unafuu wa maisha raia na mpango mpya wa kiuchumi, ambao utamkubalia aitishe msaada wa kifedha na kuiokomboa nchi hiyo kutoka kwa Shirika la Fedha Duniani IMF.



Waumini wa Kiislam wakikamilisha ibada ya Hijja kwa kupanda mlima wa Arafa nje kidogo ya mji wa Makka jana. **PICHA: REUTERS**

# Mwili wa Shinzo Abe wawasili Tokyo

**TOKYO,** JAPAN

MWILI wa Waziri Mkuu wa zamani wa Japan, Shinzo Abe umewasili nyumbani kwake katika mji mkuu wa nchi hiyo Tokyo.

Abe alipigwa risasi na kuuawa alipokuwa akihutubia katika mkutano wa kampeni ya kisiasa juzi kusini mwa mji wa Nara.

Polisi wanaochunguza mauaji yake walisema mshukiwa Yamagami aliyefyatua risasi aliwaambia maofisa kwamba alikuwa na chuki dhidi ya kiongozi huyo kupitia shirika maalum.

Walisema, mtuhumiwa Yamagami aliamini Abe alikuwa sehemu ya shirika hilo, ndiyo aliamua kumpiga risasi.

Alipoulizwa na mjumbe wa vyombo vya habari vya Japan nia ya kumpiga risasi kiongozi huyo , polisi walisema kwamba Yamagami alikiri kumpiga risasi Waziri Mkuu huyo wa zamani kwa lengo la kumuua.

Waziri Mkuu wa sasa Fumio Kishida, alitembelea eneo la tukio jana mchana.

Kulingana na taarifa za vyombo vya habari nchini humo, kutakuwa na mkesha wa maombi siku ya Jumatatu na mazishi ya Abe yatafanyika Jumanne.

Abe alikuwa Waziri mkuu aliyehudumu kwa muda mrefu zaidi nchini humo na kifo chake ambacho kimetokea akiwa na umri wa miaka 67, kimewashtua wengi katika nchi hiyo ambako visa vya uhalifu wa bunduki ni nadra kutokea.

Kiongozi huyo aliuawa alipokuwa akifanya kampeni kwa ajili ya chama chake katika uchaguzi wa bunge wa Jumapili.

# Bilionea Elumelu aanzisha mfuko wa wajasiriamali

**LAGOS,** NIGERIA

MFANYABIASHARA bilionea wa Nigeria, Tony Elumelu, kupitia Africa No Filter, amezindua mfuko maalum kwa ajili ya kuwawezesha wabunifu wa Kiafrika.

Mfuko huo uliopewa jina la Mfanyabiashara huyo unalenga kutoa fedha kwa ajili ya kuwaendeleza wajasiriamali barani Afrika.

Mfuko huo wenye kiasi cha dola 30,000 za Kimarekani umedhaminiwa na kampuni ya Heirs Insurance na Heirs Life Assurance, ambazo ni kampuni tanzu za uwekezaji ya Pan-African Investment Group inayoitwa HYPERLINK "http://www.heirsholdings.com/" \hHeirs Holdings.

Mwenyekiti wa Heirs Holdings na Mwanzilishi wa Shirika la Tony Elumelu, amekuwa kinara wa ujasiriamali barani humo.

Amewawezesha vijana ambao wamejikita katika ujasiriamali barani Afrika zaidi ya 15,000 na kugharimu kiasi cha dola milioni mia ambazo zimetengwa na shirika hilo kwa kazi hiyo.

**BBC**

MAKALA

# KUWA KIONGOZI BILA MADARAKA



Na Magabilo Masambu - 0689157789

MUSA akamwambia Mungu, mimi ni nani hata niende kwa Farao na kuwatoa wana wa Israeli watoke Misri? Naye akamjibu, nenda kwa maana nitakuwa pamoja nawe na hii itakuwa ishara kwamba, nimewabariki ninyi. Mtakapokuwa mmekwisha kuwatoa hao watu kutoka Misri, mtanitumikia juu ya mlima huu."

Hii inaitwa kuongoza bila madaraka au kuongoza bila uongozi yaani "To lead without leadership". Maana yake ni kwamba, unaweza kuwa kiongozi mzuri sana bila kuwa na madaraka kwa sababu kuna tofauti kubwa kati ya uongozi na madaraka. Kuna watu ni viongozi lakini hawana madaraka na kuna wenye madaraka wasiyo viongozi.

Musa wakati anatumwa kuwatoa wana wa Israeli katika utumwa, hakuwa na madaraka bali alikuwa kiongozi ambaye uongozi huo hakuutafuta ila Mwenyezi Mungu aliona amtumie kwa kazi hiyo baada ya kuona baadhi ya vitu ndani mwake kama vile upatanishi, upole na unyenyekevu wake katika uso wa dunia.

Wako watu wanaodhani kwamba ili kuwa viongozi ni lazima wawe na nafasi fulani za madaraka. Utasikia wakisema nikiwa fulani nitafanya hivi na vile lakini mpaka hapo alipofikia hakuwahi kufanya jambo lolote linaloashiria kwamba iwapo siku moja atapewa nafasi ya madaraka atafanya zaidi!

Uongozi huwa hausubiri nafasi ya madaraka ndiyo maana hata wanyama wawapo kwenye kundi yupo anayewaongoza wenzie lakini hatujawahi kuwaona wakifanya kampeni na hatimaye uchaguzi ili kuwapata viongozi wao badala yake utawaona tu wamejipanga na wanamfuata mmoja wao.

Huwezi kutofautisha uongozi na uanaharakati kwa sababu ukweli ni kwamba kila kiongozi ni mwanaharakati japo si kila mwanaharakati ni kiongozi mwenye madaraka. Kuna watu huwa wanadai kwamba wao si wanaharakati bali ni viongozi pengine hawaelewi dhana ya harakati. Kama umewahi kutetea jambo lolote hata linalokuhusu wewe binafsi, wewe ni mwanaharakati japokuwa unaweza kuwa si kiongozi mwenye madaraka.

Hatuwezi kuwa viongozi bora kwa kuyatafuta madaraka pekee yake. Kufanya hivyo ni kuufanya uongozi kuwa ajira ya kuchuma mali za umma na kuwaacha wananchi katika matatizo ya umaskini badala ya kuwasaidia katika kutatua changamoto zao ilihali tunatumia nafasi walizotupatia kujinufaisha sisi na familia zetu.

Viongozi wengi tulio nao kwenye jamii zetu ni wale wanaokuta mtu fulani anaonewa mahala fulani na wanapita bila kutaka kujua nini kimetokea kwa kisingizio kwamba haya hayawahusu lakini kesho na keshokutwa wanakuja kuomba nafasi za kuchaguliwa eti wakatetee haki za watu. Kama ulishindwa kumtetea huyo mmoja uliyemkuta anapigwa, utaweza kutetea kijiji, wilaya, jimbo au nchi? Tena badala ya kuingilia kati unauliza hivi hapa hakuna kiongozi wa mtaa? Unauliza hivyo halafu kesho unataka kuwa kiongozi!

Wako wanaokwenda kwa wachungaji na mashehe na wengine hata kwa waganga wa jadi wakiomba kuombewa au kuaguliwa ili kuwa viongozi. Wanachokitafuta hapo si uongozi bali madaraka. Iwapo watayapata madaraka hayo huku wakiwa si viongozi ndani mwao, lazima wananchi wategemee maumivu na mateso makali katika muda ambao watu hao watakuwa madarakani.

Kuna usemi kwamba kila mtu ni kiongozi. Hata mimi nakubaliana nao lakini swali ni je, kiongozi wa nini? Nasema hivyo kwa sababu vya kuongoza viko vingi. Si lazima ukawa kiongozi wa watu bali unaweza kuwa kiongozi wa kujiongoza mwenyewe, mifugo yako au hata mahindi shambani mwako. Kwa hiyo tusichukulie kwa ujumla wake kwamba kila mtu anaweza kuongoza ndiyo maana leo wapo watu ukiwaambia suala la kuongoza wengine watakataa kabisa, hawataki kusikia kitu kinaitwa madaraka.

Bahati mbaya tuliyo nayo, hasa Afrika, wale wanaoonekana kuwa viongozi wazuri wenye maono, wenye dhamira ya dhati kabisa wanakumbana na vikwazo vingi kwa sababu wale wenye uwezo mdogo katika madaraka wanawahofu wao. Kila wanapojitahidi kunyanyua vichwa vyao, vinagongwa na kuhakikisha hawasimami.

Ukweli ni kwamba viongozi wengi waliofikia mafanikio makubwa katika nyanja hiyo ukiwauliza watakwambia wamepitia mengi magumu. Hii si kwenye uongozi tu bali jambo lolote lenye mafanikio lina mitihani migumu sana. Niwatie moyo tu wale wote wenye hofu ya kuyafikia mafanikio yenu mtayafikia na mnapoona dalili za kukata tamaa, mafanikio yako karibu, msirudi nyuma kwa sababu binadamu si anayeamua hatima ya mtu mwingine, bali anayo nafasi ya kuichelewesha na mwisho wa siku yatatimia.

Wale wote wenye nia ya kuwa viongozi wa kesho, tusihangaike kuyatafuta madaraka bali tuonyeshe njia pale tulipo si kwa lengo la kujionyesha bali kuwasaidia watu ili wayafikie malengo yao kama ambavyo sisi pia tumesaidiwa na wengine. Tusingoje vipindi vya uchaguzi na kujipeleka kwa watu. Waache watu wenyewe watupeleke kwenye hizo nafasi kutokana na maisha yetu ya kila siku kama ambavyo Musa alipelekwa na Mungu kuwakomboa wana wa Israeli kutoka utumwani.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kwaheri John Makelele, mchezaji uliyenusuru Simba kushuka daraja



Na Adam Fungamwango

ASUBUHI ya Julai 23, 1988 kulikucha kama kunavyokucha siku zingine. Kwa watu wengine ilikuwa siku ya kawaida tu wala hakukuwa na kitu chochote cha muhimu. Waliendelea na kazi zao kama kawaida. Kwa mashabiki, wapenzi na wanachama wa klabu za Simba na Yanga, ilikuwa siku muhimu mno.

Jioni yake kulikuwa na mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga ikichezwa kwenye Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam (sasa Uhuru). Wanachama na mashabiki wa Yanga walikuwa wanaombea timu yao ishinde au itoe sare ili itwae ubingwa.

Ingawa mechi ya watani wa jadi haitabiriki, walikuwa na matumaini makubwa zaidi kutokana na kwamba ulikuwa mwaka mbaya zaidi kwa Simba kwani ilihitaji ushindi ili kubaki Ligi Kuu (zamani Ligi Daraja la Kwanza). Simba haikuhitaji hata sare kwenye mechi hiyo, kwani kwa sare yoyote ilikuwa inateremka daraja.

Ilikuwa ina pointi 18, hivyo ilihitaji pointi mbili ifikishe pointi 20 ili iizidi Tukuyu Stars ambayo ilikuwa na pointi 17 na ilibakisha mechi moja dhidi ya Coastal Union. Ikumbukwe kuwa zamani timu ikishinda inapata pointi mbili tu na si tatu kama sasa.

Kutokana na hali hiyo, Simba ilitakiwa kuifunga Yanga ili imalize ligi ikiwa na pointi 20, ili hata kama Tukuyu Stars ingeifunga Coastal Union imalize ikiwa na pointi 19 tu. Ligi hiyo ilikuwa na timu 12, huku Reli ya Morogoro ikiwa imeshateremka daraja na pointi zake 13, hivyo ilihitajika nyingine moja ishuke nayo.

Wakati Simba ikitakiwa lazima ishinde, Yanga ilihitaji sare tu ili iwe na pointi 27 na kutawazwa ubingwa, kwani zisingefikiwa na timu yoyote ile, achilia mbali ushindi.

Muda ulifika, wachezaji wa pande zote mbili walijipanga uwanjani na kipute kikaanza saa 10:00 jioni.

Alikuwa Edward Chumila (marehemu), aliyewainua mashabiki wa Simba uwanjani, alipopachika bao la kwanza kwa Simba dakika ya 21 na kuipa matumaini ya kubaki kwenye ligi.

Dakika 15 baadaye, yaani dakika ya 36, Issa Athumani (marehemu), aliisawazishia Yanga bao na hadi mapumziko timu hizo zikaenda vyumbani zikiwa sare ya bao 1-1. Ni matokeo ambayo bado yalikuwa mazuri kwa Yanga, kwani yangeweza kuipa ubingwa na kuishusha Simba daraja.

Dakika ya 13 kipindi cha pili, sawa na dakika 58 ya mchezo mzima, John Makelele 'Zig Zag', straika hatari wakati huo aliyesajiliwa na Simba kutoka Pamba, aliukwamisha mpira ndani ya wavu na kuandika bao la pili la ushindi na matokeo hayo yakasimama hadi mwisho.

Ni krosi ya chini ya Malota Soma ambayo Sahau Kambi alitaka kudaka au kuuokoa, lakini Makelele aliuwahi na kuudokoa, ukampita juu ya mbavu zake, lakini haukwenda mbali, bali ulikuwa nyuma yake. Makelele alimruka Sahau na kuwahi, akaukwamisha wavuni.

Ni bao ambalo litabaki kwenye kumbukumbu ya vitabu vya historia ya Simba na soka la Tanzania kwa ujumla kwa sababu iliifanya timu hiyo kusalia Ligi Kuu.

Ni kipindi ambacho Simba ilipitia wakati mgumu kwa misimu mitatu mfululizo 1987, 1988 na 1989 ikinusurika kushuka daraja, kutokana na mgogoro mkubwa wakati huo wa pande mbili za wanachama na viongozi.

Upande mmoja ulimuunga mkono Katibu Mkuu wa zamani wa klabu hiyo, Jimmy David Ngonya 'Gorbachev', na upande mwingine ulikuwa wa Baraza la Wazee la klabu hiyo.

Hata kikosi hicho kiligawanyika sehemu mbili, hivyo kukawa na kuhujumiana pia.

Kufungwa kwa Yanga mabao 2-1 dhidi ya Simba kuliifanya Coastal Union kuizidi Yanga pointi moja na kuwa bingwa.

Makelele ambaye alikuwa shujaa kwenye mechi hiyo alifariki dunia Jumamosi ya Julai 2, mwaka huu, ikikaribia miaka 34 tangu alipofanya tukio hilo la kihistoria.

Kwa mujibu wa mkewe, Salome Makelele, mumewe alifariki dunia kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili, jijini Dar es Salaam na kuzikwa Jumanne wiki hii nyumbani kwao, kijiji cha Mtakuja, Moshi mkaoni Kilimanjaro.

Makelele ambaye pia aliichezea timu ya taifa, Taifa Stars, alikuwa ana uwezo wa kucheza kama straika na winga wa kulia.

Alikuwa na mbio pamoja chenga za maudhi akizipiga kwa staili ya aina yake, kiasi cha mashabiki wa soka wakampachika jina la 'Zig Zag'. Hiyo ni kutokana na aina ya upigaji wake wa chenga.

Baada ya mechi hiyo, Sahau aliondolewa uwanjani akilindwa na askari wa kikosi cha mbwa na farasi kutokana na mashabiki wa Yanga kutaka kumpiga kwani kwa tafsiri yao alifungwa bao hilo kizembe au 'kuna namna'.

Kutokana na varangati kubwa lililotokea, gazeti la mfanyakazi wakati huo ambalo lilikuwa likitoka kila Jumamosi, lilitoa picha kipa huyo wa Yanga akisindikizwa na askari wakiwa wamemzunguka huku kukiwa na kichwa cha habari juu 'ambavyo Sahau hatasahau.'

Makelele alikuwa kipenzi cha mashabiki wa Simba miaka hiyo kwani alikuwa kama mkombozi akifunga mabao mengi ya timu hiyo, au kutoa pasi za mwisho.

Kutokana na Simba kuwa na mastraika wengi kama Edward Chumila, Malota Soma na Zamoyoni Mogella, wakati mwingine Makelele alikuwa akianzia benchi na kuingia kipindi cha pili.

Kila anapoingia, vitu anavyofanya mara nyingi Simba ilikuwa ikipata bao kwa kufunga mwenyewe au kutoa pasi ya mwisho. Ndiyo maana kila anaposimama akitaka kuchukua nafasi ya mtu siku ambayo ameanzia benchi, uwanja mzima ulikuwa unasimama na kushangilia.

Hapo ndipo mtangazaji nguli wa mpira wa miguu wakati huo husema: "Wasikilizaji, Makelele hayo mnayoyasikia, kuna mtu moja huku nje anaitwa John Makelele, anapiga jaramba."

Kazi kubwa ameifanya. Kwaheri Makelele, uliyeinusuru Simba kushuka daraja.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na walipomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-9

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ALIPOHAKIKISHA wote wameingia kwenye gari akajipigia makofi kimoyomoyo. Hakuwa na haraka, aliliacha litangulie na yeye kuanza kulifuata kwa mbali. Bahati nzuri aliyoipata ni kwamba magari mengi yalikuwa yameshatangulia kuondoka. Gari la Nassor na Nassir yalikuwa kati ya yale machache yaliyobaki. Aliwasha pikipiki yake na kuanza kuifuata kwa kasi. Kila kitu alishakipanga na mpaka eneo la kufanya tukio.

Gari hilo lilikuwa likitoka Tuangoma kwenda Kongowe. Kabla ya kufika huko katikati kuna kona pamoja na mteremko mkali wenye korongo kubwa linalotenganisha Kigamboni na Kongowe na Mbagala.

Ndilo eneo ambalo alilihitaji zaidi kutekeleza alichoagizwa na baba yake.

Spidi ya pikipiki aliyokuwa akiendesha ilizidi mara mbili ya gari walilokuwa Nassor na Hassan. Na walipozidi kulikaribia eneo hilo, ndipo alipozidi kuongeza mwendo.


Mita chache kabla gari hilo kuingia kwenye mteremko mkali, Prince alijipapasa kifuani kwenye koti alilovaa na kutoa bastola yake kwa mkono wa kushoto.

Mkono wa kulia ulikuwa umeshikilia upande mmoja wa pikipiki. Hakuwa na wasiwasi kwa sababu michezo hiyo ya hatari ilikuwa ni sehemu ya maisha yake.

Taa za pikipiki aliyokuwa akiendesha, alizielekeza kwenye magurudumu ya nyuma ya gari lililokuwa mbele yake.

Bastola yale aliilenga kwenye gurudumu la nyuma la mkono wa kushoto. Akaachia risasi mbili. Prince anaweza kukosea vitu vingine, lakini si shabaha. Tangu mdogo kazi yake ni hiyo tu. Risasi zilifanya kazi iliyokusudiwa. Zikapasua tairi la nyuma, wakati gari likiwa liko kwenye mteremko mkali.

Gari liliyumba na kuanza kupoteza uelekeo. Wakati huo Prince alikuwa mita zipatazo 30 hivi kutoka kwenye gari la mbele. Kutokana na kasi kubwa lililokuwa nayo, dereva alionekana kushindwa kulidhibiti, hivyo kuyumba kulizidi.




**Gari liliyumba na kuanza kupoteza uelekeo. Wakati huo Prince alikuwa mita zipatazo 30 hivi kutoka kwenye gari la mbele. Kutokana na kasi kubwa lililokuwa nayo, dereva alionekana kushindwa kulidhibiti, hivyo kuyumba kulizidi.**

Alipiga nyingine moja kwenye tairi la nyuma la upande wa kulia. Matairi yote ya nyuma sasa yalikuwa yamepasuka. Wakati gari lilikuwa likiyumba, sasa lilishindwa kudhibitiwa, likagonga ukingo wa barabara na kupaa juu mithili ya ndege, kabla ya kubiringika mara mbili juu, huku likitua chini. Lakini tayari lilikuwa nje ya barabara, hivyo kuangukia kwenye korongo.

*******************************

"Ni kama vile tumemaliza kazi mwanagu. Iliyobaki si kubwa sana kama ulizozifanya." "Kwa nini unasema hivyo baba?" "Tayari wote wanne, Sabri, Hussein, Nassor na Hassan, wameshakuwa marahemu, bado mmoja tu."

"Usiseme hivyo baba, huyo wa mwisho anaweza kuwa kikwazo kwetu." Prince alitahadharisha. Baba yake alimtazama jicho kali, ambalo lilionyesha kuwa amekasirishwa na jibu lile.

"Nilikwambia, sisi kushindwa kwetu ni mwiko ndiyo maana hadi leo hii Jeshi la Polisi halijaweza hata kunusa harufu ya muuaji, achilia mbali kumkamata." Prince hakujibu kitu, alikaa kimya, akimtazama mzee Pokwa aliyeonekana kuongea kwa hasira kidogo.

"Hivi unajua ukishammaliza huyu unakuwa ndiyo mwisho wa kisasi chetu?"

"Ndiyo baba."

"Na wewe na mimi tunaishi kwa raha bila wale watu waliokuwa tishio kwangu na kwako?"

"Ndiyo." "Na ndiyo waliohusika kula njama kumdhulumu mama yako mali zake, mashamba, ardhi halafu wakamuua?" "Najua baba."

"Kama umewamaliza hawa wote ambao walikuwa wagumu sana, utamshindwa huyu wa mwisho?"

"Ni nani kwani huyu baba?"

"Ni mwanamke. Huyu ndiye mwanamke pekee kwenye orodha hii! Baada ya kummaliza nitakwambia alivyohusika kwenye tukio hili. Wakati ule alikuwa msichana, lakini kwa sasa ni mama mtu mzima. Je, umewaweza hawa, unashindwa huyu mama mtu mzima, unayeweza kumzimisha hata kwa mikono bila kutumia hata bastola yako?" "Kama hivyo ni kweli baba. Itakuwa ni rahisi tu."

"Vizuri, sasa nisikilize. Kabla sijakupa picha zake. Ninazo zote mbili, moja akiwa msichana na nyingine ya hivi karibuni. Anaitwa Hidaya. Anaishi Mwananyamala Kisiwani. Sehemu yenyewe inaitwa Maduka Matatu. Ukifika Jengo la Serikali za Mitaa kuna kona, upande wa kushoto kuna zahanati. Nyumba inayotizamana na hiyo zahanati ndiyo anayoishi huyo mama.

"Kwa bahati nzuri huhitaji kuwapita watu wengi ili kukutana naye. Ua wake umezungushwa kwa matofali makuukuu, mlango wake ni wa bati. Ukiingia unakutana na nyumba ndogo tu ya vyumba viwili na sebule. Si ya kupanga wala nini. Usiku ni sehemu nzuri ya kwenda kumaliza kazi yako kabla hajalala. Na si usiku mkubwa sana, kule ni uswahilini, saa tatu watu bado wapo macho hawajalala. Wapo nje wanapunga upepo, au wapo ndani wanaangalia TV."

"Sawa baba nimekuelewa, Sabri na Hussein nilitumia mbinu zinazofanana, Hassan na Nassor nilitumia mbinu tofauti, sasa hii inaonekana nitatumia mbinu tofauti zaidi, niachie hili."

"Ahsante sana mwanangu, ndoto za muda mrefu, za miaka mingi sasa zimekamilika."

*************************

Alipaki gari lake maeneo ya wazi Mwananyamala Mwinjuma. Akaanza kutembea kwa miguu, kukatiza Kanisa la Pentekoste, Manjawila, hadi Maduka Matatu. Hakuwa mwenyeji sana huko, ila aliifuata barabara iliyokuwa ikielekea Kwa Kidile na kushuka Bonde, kabla ya kupandisha maeneo ya Magomeni Makanya.

Aliambiwa akifika Maduka Matatu mbele kuna Jengo la Serikali za Mitaa. Na kweli baada ya kutembea kwa muda kidogo alikutana na maandishi hayo. Na hapo hapo kulikuwa na kona, iliyoacha barabara kubwa na kuingia njia ndogo, lakini iliyoweza kupitisha hata gari ndogo.

Nyumba ya kwanza tu kushoto alikutana na maandishi mengine, ikionyesha ni jengo la zahanati. Akakumbuka aliambiwa nyumba ya Hidaya inapakana na zahanati hiyo upande wa kulia kwake. Ilikuwa ni saa 2:30 usiku. Prince aliwahi zaidi kuliko muda alioambiwa kuutumia kuifanya kazi hiyo.

Muda atakaoutumia kwanza ni kusoma mazingira na kuangalia aingie vipi? Alijipitisha na kwenda mbele, halafu akarudi na kukaa kwenye benchi nje, akijifanya ni mmoja wa watu wanaosubiri huduma ya kutibiwa.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# BI HINDU HATUNAYE

## KAONDOKA NA UCHESHI, MISEMO YA KISWAHILI

MUASISI wa michezo ya kuigiza, Chuma Selemani, maarufu zaidi kama Bi Hindu amefariki Dunia asubuhi ya jana.

Kulingana na taarifa zilizothibitishwa na baadhi ya ndugu zake, Bi Hindu, alifariki akiwa nyumbani kwake Magomeni jijini Dar es Salaam, baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Msanii huyo mkongwe alikua akisumbuliwa na maradhi ambayo yalimfanya kulazwa hospitali na kisha kurudi nyumbani kwake akiendelea kupata matibabu.

Bi Hindu ambaye anakumbukwa kutokana na ucheshi na maneno yake ya uswahilini, amekuwa katika tasnia ya uigizaji tangu miaka ya 70 katika kituo cha redio Tanzania Dar es Salaam(RTD).

Baada ya kuanzishwa kwa vituo binafsi vya televisheni, Bi Hindu na wenzake waliunda kundi la Kaole ambalo lilifanya kazi na kituo cha ITV kwa kuonyesha tamthilia zao mbalimbali.

# Daniesa yamkuta mbele ya Gwajima

Mwimbaji anayekuja kwa kasi kutoka Shinyanga, Daniesa Malula, amejikuta aking'ang'aniwa na mashabiki mbele ya Askofu Josephat Gwajima katika uwanja wa Kambarage wiki hii.

Akizungumza na BT Daniesa, amesema alijikuta kwenye wakati mgumu baada ya mashabiki kutaka arudie kuimba nyimbo zake baada ya kupewa nafasi ya kuimba kwenye mkutano ulioandaliwa na Gwajima mjini humo.

"Wimbo wangu wa Madhabahu umewabariki wengi, watu walijikuta wananing'ang'ania ili niurudie tena kwenye mkutano mkubwa wa Gwajima uliofanyika hapa Shinyanga," amesema Daniesa.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DI MARIA RASMI MALI YA JUVENTUS

●●●Amekuwa nyota wa kwanza kutua Turin huku wengine akiwamo...

**TURIN, ITALIA**

KLABU ya Juventus imemfanya Angel Di Maria kuwa mchezaji wao wa kwanza wa usajili wa hali ya juu bila malipo msimu huu, huku Paul Pogba akitarajiwa kufuata.

Kibibi kizee hicho cha Turin kinasifika kwa ustadi wake wa kuchukua mastaa walio huru na Di Maria mwenye umri wa miaka 34, anakuwa mchezaji wa karibuni zaidi kusaini mkataba wa mwaka mmoja.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina aliondoka Paris Saint-Germain, ambako alikaa kwa miaka saba, mwishoni mwa msimu huu.

Di Maria alishinda mataji matano ya Ligue 1 akiwa na Les Parisiens hao, pamoja na mataji mengine 13.

Hata hivyo, taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya liliwakwepa PSG na Di Maria.

Katika msimu wake wa mwisho katika mji mkuu wa Ufaransa, Di Maria aliona muda wake wa kucheza ukipunguzwa.

Alianza mara 19 tu katika mechi za Ligue 1 - na mara 22 pekee katika mashindano yote - akichangia jumla ya mabao matano na asisti nane.

Kwa kusajiliwa na Bianconeri hao kwa uhamisho huo, Di Maria anafuata nyayo za Pogba, Andrea Pirlo, Aaron Ramsey, Adrien Rabiot, Sami Khedira na Dani Alves.

## KWA UFUPI

### RONALDO BADO HAKIJAELEWEKA
HUKU kukiwa na uvumi unaoendelea kuongezeka kuhusu hali ya baadaye ya mashambuliaji Mreno mwenye umri wa miaka 37, Cristiano Ronaldo, kocha wa Manchester United, Erik ten Hag ametambua haja ya kuimarisha safu ya ushambaluaji ya timu yake. ***(Manchester Evening News)***

### UNITED KUSAJILI KINDA
Erik Ten Hag ana matumaini ya kumsajili mshambuliaji raia wa Uholanzi, Brian Brobbey mwenye umri wa miaka 13 kutoka RB Leipzig kwa pauni milioni 13. ***(Times)***

### MARTINEZ AKARIBIA UNITED
KLABU ya Manchester United wameboresha ofa yao kwa ajili ya mlinzi wa Ajax mwenye umri wa miaka 24, Lisandro Martinez katika juhudi za kuipiku Arsenal katika kupata saini ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina. ***(Mail)***

### ARSENAL YAMFUATA PAQUETA
KLABU ya Arsenal ina ya kumsajili kiungo wa kati wa Lyon mwenye umri wa miaka 24, Lucas Paqueta, ambaye amekuwa akihusishwa na taarifa za kuhamia Newcastle.***( Foot)***

### ZIYECH AMTEMA WAKALA
NYOTA wa Chelsea, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 29, ambaye amekuwa akihusishwa na AC Milan, ametangaza uamuzi wake wa kuachana na wakala wake, Nakhli Mondial baada ya miaka 12. ***(Ziyech's Instagram)***

### RAPHINA KUTUA BARCA
BARCELONA wamewasilisha 'ofa ya mwisho' ya pauni milioni 47 kwa ajili ya Raphinha mwenye umri wa miaka 25- ambaye amekuwa akihusishwa na klabu za Chelsea na Arsenal. ***(Sport)***

### BARCA KUMBAKISHA DEMBELE
KOCHA wa Barcelona, Xavi anataka kumpa mkataba mpya winga Mfaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 25, ambaye ni mchezaji huru baada ya mkataba wake katika pale Nou Camp kumalizika. ***(Mirror)***

### KLUIVERT ANUKIA WEST
KLABU ya West Ham inaangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa AS Roma, Justin Kluivert mwenye umri wa miaka 23, kwa hadi pauni milioni 13. ***(Gazzetta dello Sport via Team Talk)***

### BENNACER KUTUA ARSENAL
ARSENAL inmeonyesha nia katika kumsajili kiungo wa kati raia wa Algeria, Ismael Bennacer mwenye umri wa miaka 24 kutoka AC Milan. ***(Calciomercatoweb)***

### ZAHA ANUKIA AS ROMA
AS Roma wanaangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Crystal Palace na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 29. ***(Fabrizio Romano)***

### ARIBO MAMBO MAZURI
KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Joe Aribo mwenye umri wa miaka 25 yuko karibu kujiunga na Southampton kutoka Rangers kwa mkataba wa awali wa pauni milioni sita. ***(Fabrizio Romano)***

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
HAUGESUND
VERSUS
HAM-KAM
1 | 2.07
X | 3.42
2 | 3.32

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
GBT:0249

# BARCELONA YAFANIKIWA KUMBAKISHA DEMBELE



**BARCELONA, Hispania**

NYOTA Ousmane Dembele anakaribia kusaini mkataba wa miaka miwili na Barcelona, huku winga wa Leeds United, Raphinha akikaribia kutua klabuni hapo, kwa mujibu wa 90min.

Vichwa vya habari vya dirisha la usajili la majira haya ya joto vimetawaliwa na Barcelona, ambao licha ya kuwa na msukosuko wa kifedha, wanahusika katika mikataba kadhaa ya wachezaji bora zaidi duniani.

Majadiliano yanaendelea na Manchester United kuhusu uwezekano wa kuuzwa kwa Frenkie de Jong, na ingawa Rais, Joan Laporta amesisitiza hataki kumwachia Mholanzi huyo, kuondoka kwake kunaweza kuwa msingi wa kufungua mikataba mingine kadhaa kwa Barca.

Miongoni mwa vipaumbele vya wababe hao wa Katalunya ni kumsajili, Robert Lewandowski kutoka Bayern Munich, lakini pia kumekuwa na msisitizo mpya katika wiki za hivi karibuni kuhusu kumbakisha Dembele.

Winga huyo wa kimataifa wa Ufaransa pale Camp Nou amekuwa akipanda na kushuka na imeonekana ana uhakika miezi kadhaa ijayo angeondoka katika klabu hiyo kama mchezaji huru.

Chelsea imekuwa ikiongoza katika kinyang'anyiro cha kuwania saini yake, huku kocha, Thomas Tuchel akihitaji kuimarisha safu yake ya ushambuliaji, lakini kuingilia kati kwa muda kutoka kwa kocha wa Barcelona, Xavi kumeifanya klabu hiyo kufanya kila iwezalo ili Dembele abaki.

Baada ya mazungumzo ya mara kwa mara, 90min inaelewa mkataba wa miaka miwili juu ya mshahara uliopunguzwa sasa umekubaliwa.

Masharti ya kibinafsi yamekubaliwa kwa muda mrefu kati ya Raphinha na wakala wake Deco, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amekuwa akisubiri Barcelona kutafuta njia ya kufadhili dili hilo.

# Madrid yajiandaa kumuuza Jovic

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid imethibitisha imekubaliana na Fiorentina inayoshiriki Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa ajili ya kumuuza mshambuliaji, Luka Jovic.

Mshambuliaji huyo wa Serbia alikuwa bora wakati wa enzi zake Eintracht Frankfurt, huku mabao 17 ya Bundesliga msimu wa 2018/19 yakitosha kuwashawishi Los Blancos hao kumsajili kwa euro milioni 60.

Hata hivyo hakuwahi kupata mfululizo wa mechi, mara chache hakuaminiwa na Zinedine Zidane au Carlo Ancelotti katika kikosi chao cha kwanza.

Alirejea Frankfurt kwa mkopo msimu uliopita lakini sasa ameondoka Bernabeu kabisa, na kusaini mkataba wa miaka miwili na Fiorentina.

Taarifa ya Real ilisema: "Real Madrid C. F. na ACF Fiorentina wamekubaliana dili la uhamisho wa Luka Jović

"Klabu yetu inapenda kutoa shukrani zake kwa kazi yake na kujitolea wakati alipokuwa Madrid, ambapo ameshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, mataji mawili ya LaLiga na mawili ya Super.

"Real Madrid inamtakia kila la heri yeye na familia yake katika kipindi hiki kipya cha maisha yake."

Jovic anatarajiwa kuingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza cha Fiorentina, huku klabu hiyo ikipania kuimarika baada ya kumaliza nafasi ya saba kwenye Serie A msimu uliopita.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# BI. HINDU KUZIKWA LEO, SIMBA, WASANII WAMLILIA

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

MSANII mkongwe wa maigizo na filamu nchini, Chuma Selemani maarufu Bi. Hindu amefariki dunia na anatarajiwa kuzikwa leo kwenye makaburi ya Mwinyimkuu yaliyopo Magomeni jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Bi. Hindu ambaye alikuwa mwanachama mkongwe wa klabu ya Simba, alifariki dunia jana asubuhi akiwa nyumbani kwake Mtaa wa Uweje Magomeni Mapipa baada ya kusumbuliwa na maradhi ya kupooza kwa muda mrefu. Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Chama cha Waigizaji Tanzania, Salum Mchoma 'Chiki' alisema mazishi ya msanii huyo mkongwe yatafanyika saa saba mchana.

"Bi. Hindu ameacha watoto wanne na wajukuu kadhaa ambao kwa sasa hatuna idadi kamili, tunatarajia mwili wake utaendaa kupumzishwa katika makaburi ya MwinyiMkuu, hapa Magomeni jirani na alipokuwa anaishi, " alisema Chiki.

Alisema msiba huo ni pigo kwa familia ya msanii huyo kwa sababu alikuwa ni mshauri mkubwa kwa jamii yake lakini pia kwa wasanii wa filamu kutokana na uongwe wake kwenye tasnia hiyo.

Enzi za uhai wake alishawahi kufanya kazi na waigizaji mbalimbali wakiwemo marehemu, Amri Athumani 'Mzee Majuto', Shamsa Ford, Jacob Stephen 'JB' na Wema Sepetu.



JB aliliambia gazeti hili marehemu alikuwa mmoja kati ya waigizaji nyota na gwiji katika tasnia hiyo lakini pia mwalimu kwa wasanii chipukizi.

Alisema katika kipindi chote cha uhai wake, Bi. Hindu alikuwa akisimamia weledi katika kazi za sanaa lakini pia akisisitiza nidhamu kwa watu wa karibu yake.

"Kwangu alikuwa mama na rafiki nilipata bahati ya kushirikiana nae katika filamu tatu ambazo ni 'Shikamoo Mzee', 'Zawadi Yangu' na 'Wageni Wangu' ambazo zilipamba vizuri, " alisema JB.

Mwenyekiti wa zamani wa Simba, Hassan Dalali amesema amezipokea kwa masikitiko taarifa za msiba wa Bi. Hindu ambaye alikuwa anaifahamu kiundani klabu hiyo tangu ilipoanzishwa mwaka 1936.

"Tumepoteza mtu muhimu kwenye klabu yetu, alikuwa anajua kumbukumbu zote za Simba, vilevile alikuwa ni mwanachama aliyeumia kwa ajili ya timu yake," alisema Dalali.

Mwenyekiti huyo alisema kuanzia miaka ya 1970-1980, alikuwa anawapikia wachezaji chakula nyumbani kwake kikiwamo kubeba karai la kokoto wakati jengo lao la Kariakoo lilipokuwa linajengwa.

"Hakuwa mwoga, alitoa mawazo yake pale alipoona mambo hayaendi vizuri, alikuwa ni kiungo kati ya wazee, vijana na uongozi, tunamshukuru Mungu kwa maisha yake yote," Dalali alisema.



Baadhi ya wanachama wa Yanga wakisubiri matokeo ya uchaguzi mkuu wa klabu yao uliofanyika jana jijini Dar es Salaam. Hersi Said alichaguliwa bila kupingwa kuwa mwenyekiti mpya wa klabu hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba U-20 yaichapa Yanga

**Na Adam Fungamwango**

TIMU za soka za vijana wa umri chini ya miaka 20 za Simba na Mtibwa Sugar zinaendelea kutamba katika Ligi Kuu ya U-20 inayoendelea hapa jijini Dar es Salaam.

Kikosi cha Simba kinaongoza kwenye Kundi A baada ya juzi kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya yosso wenzao wa Yanga.

Wekundu hao wa Msimbazi wamefikisha pointi sita baada ya kushinda mechi zote mbili walizocheza huku Mtibwa Sugar ikiongoza kwenye Kundi B, ikiwa nayo imeshinda mechi zote mbili ilizocheza.

Kwa mujibu wa msimamo uliotolewa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), wakati timu hizo zikiongoza kwenye makundi hayo, Azam FC inaongoza katika Kundi C ikiwa na pointi nne huku KMC yenye pointi nne ikiwa kileleni katika Kundi D.

Polisi Tanzania U-20 iliyoko katika Kundi A inashika nafasi ya pili kwa kuwa na pointi tatu wakati Biashara United na Namungo zinafuatia, zote zikiwa na pointi moja kila moja.

Mbeya Kwanza iko kwenye nafasi ya pili kwenye Kundi B linaloongozwa na Mtibwa Sugar yeny pointi nne, Dodoma Jiji ya tatu ikiwa na pointi moja na Ruvu Shooting inashika mkia ikiwa haina pointi. Yosso wa Yanga wanakamata nafasi ya pili ikiwa na pointi tatu kwenye Kundi D, ambalo kinara wake ni KMC, Kagera Sugar nafasi ya tatu kwa pointi mbili na ya mwisho ni Geita Gold yenye pointi moja.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA


MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 10/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1459 | Avispa Fukuoka vs Kyoto Sanga | 2.03 | 2.94 | 3.73 |
| 13:00 | 1586 | Sagan Tosu vs Kashiwa Reysol | 2.29 | 3.04 | 2.99 |
| 13:00 | 2065 | Cerezo Osaka vs Yokohama F Marinos | 3.19 | 3.38 | 2.04 |
| 13:00 | 3970 | Urawa Red Diamonds vs FC Tokyo | 1.91 | 3.25 | 3.74 |
| 13:30 | 2864 | Chungnam Asan vs Jeonnam Dragons | 2.28 | 3.05 | 3.00 |
| 14:00 | 2688 | Jonkopings Sodra vs Ostersunds | 2.04 | 3.51 | 3.51 |
| 16:00 | 1379 | Utsiktens BK vs Osters IF | 2.77 | 3.23 | 2.57 |
| 16:00 | 3233 | Sandnes Ulf vs Ranheim | 2.55 | 3.43 | 2.41 |
| 16:00 | 3548 | Elfsborg vs AIK Football | 2.11 | 3.25 | 3.15 |
| 16:00 | 4158 | Stjordals-Blink vs Raufoss | 3.15 | 3.54 | 2.00 |
| 16:00 | 4216 | Brann vs Stabaek | 1.64 | 3.73 | 4.51 |
| 16:00 | 4661 | Seinajoen JK vs Honka | 3.20 | 3.10 | 2.15 |
| 16:00 | 5166 | Mjallby vs BK Hacken | 3.52 | 3.33 | 1.94 |
| 16:00 | 5287 | KuPS Kuopio vs Lahti | 1.39 | 4.43 | 6.50 |
| 17:00 | 4560 | Peterhead vs Aberdeen | 7.07 | 5.50 | 1.29 |
| 17:00 | 5637 | Coritiba vs Juventude RS | 1.95 | 3.19 | 3.63 |
| 18:00 | 5677 | Skovde Aik vs Orgryte IS | 2.48 | 3.41 | 2.75 |
| 18:30 | 1575 | Pepo Lappeenranta vs PK-35 | 2.85 | 3.20 | 2.29 |
| 18:30 | 2035 | Kalmar vs Sirius FK | 1.62 | 3.67 | 4.80 |
| 18:30 | 3020 | Lokomotive Sofia vs Cherno More | 3.79 | 3.15 | 1.93 |
| 19:00 | 1257 | Lillestrom vs Viking | 2.14 | 3.47 | 3.12 |
| 19:00 | 2262 | Sandefjord vs Aalesunds | 2.67 | 3.43 | 2.45 |
| 19:00 | 2467 | Rosenborg vs Jerv | 1.28 | 5.61 | 8.61 |
| 19:00 | 2669 | Valerenga vs Kristiansund | 1.48 | 4.42 | 5.83 |
| 19:00 | 4588 | Molde vs Tromso | 1.59 | 4.12 | 4.93 |
| 19:30 | 2146 | Santiago Wanderers vs Deportes Temuco | 1.95 | 3.20 | 3.64 |
| 19:30 | 2788 | Arturo Fernandez Vial vs Deportes Recoleta | 1.98 | 3.25 | 3.70 |
| 20:00 | 1786 | Deportivo Toluca vs Club Atlas | 2.92 | 3.12 | 2.43 |
| 21:00 | 2312 | Radnik Surduluca vs FK Mladost Gat Novi Sad | 1.97 | 3.40 | 3.60 |
| 21:00 | 3057 | Red Star Belgrade vs Radnicki Nis | 1.15 | 6.46 | 12.72 |
| 21:00 | 3569 | Atletico Grau vs Alianza Lima | 4.22 | 3.48 | 1.74 |
| 21:00 | 4440 | Instituto Cordoba vs San Martin SJ | 2.11 | 2.95 | 3.49 |
| 21:00 | 5067 | CSKA Sofia vs Arda Kurdzhali | 1.43 | 4.12 | 6.28 |
| 21:00 | 5162 | Sacachispas FC vs Chaco For Ever | 3.67 | 2.99 | 2.03 |
| 21:00 | 5771 | Haugesund vs Ham-Kam | 2.07 | 3.42 | 3.32 |
| 21:00 | 5807 | Vojvodina vs FK Napredak | 1.76 | 3.29 | 4.42 |
| 21:15 | 2427 | Carlos Mannucci vs FBC Melgar | 3.54 | 3.39 | 1.92 |
| 21:30 | 1274 | Racing Club vs Independiente | 1.93 | 3.15 | 3.79 |
| 22:00 | 1201 | Atletico Bucaramanga vs Rionegro Aguilas | 2.28 | 2.95 | 3.10 |
| 22:00 | 1469 | Deportivo Cali vs Jaguares de Cordoba | 1.86 | 3.24 | 3.92 |
| 22:00 | 1652 | Mitre SdE vs San Telmo | 1.61 | 3.74 | 4.72 |
| 22:00 | 1722 | Independiente DV vs Cumbaya FC | 1.22 | 5.28 | 10.76 |
| 22:00 | 2246 | Nacional Potosi vs The Strongest | 2.14 | 3.50 | 3.05 |
| 22:00 | 2576 | Corinthians vs Flamengo | 2.90 | 3.04 | 2.35 |
| 22:00 | 3038 | Antofagasta vs Univ de Chile | 2.38 | 3.10 | 2.80 |
| 22:00 | 3098 | La Equidad vs Independiente Santa Fe | 2.41 | 2.90 | 2.95 |
| 22:00 | 3129 | CA Boston River vs Defensor Sporting | 2.50 | 3.04 | 2.70 |
| 22:00 | 4000 | Estudiantes Rio Cuarto vs Gimnasia Jujuy | 1.99 | 3.00 | 3.79 |
| 23:00 | 4935 | Asociacion Deportiva Tarma vs FC Carlos Stein | 1.70 | 3.57 | 4.30 |
| 23:30 | 3027 | Universitario vs Academia Cantolao | 1.40 | 4.31 | 6.47 |

Michezo
Jumapili Julai 10, 2022
Nipashe



## Di Maria rasmi mali ya Juventus

UKURASA 21




Rais mpya wa Yanga Injinia, Hersi Said akipongezwa na Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba baada ya kutangazwa rasmi mshindi wa nafasi hiyo katika uchaguzi mkuu wa klabu hiyo uliofanyika kwenye Ukumbi wa mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni George Mkuchika ambaye ni mwanachama wa Yanga. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kichuya arejea nyumbani

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI ikimtambulisha rasmi mshambuliaji, Habibu Kyombo ni mali yake, winga, Shiza Kichuya kutoka Namungo FC anatajwa amerejea kwa Wekundu wa Msimbazi.

Kichuya alikuwa mchezaji huru baada ya mkataba wake na Namungo ya Lindi kubakiza siku chache.

Taarifa zilizopatikana kutoka kwa viongozi wa Simba zinasema Kichuya amerejea klabuni hapo baada ya kuonyesha kiwango bora katika msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliomalizika hivi karibuni.

"Ndio amerejea nyumbani (Simba), kila kitu kimeshakamilika," kilisema chanzo chetu.

Mbali na Kyombo aliyesaini mkataba wa miaka miwili, Simba imeshamtambulisha Moses Phiri kutoka Zambia na inatarajia kuanza maandalizi ya msimu mpya keshokutwa.

Simba pia inatarajia kuelekea Misri kuweka kambi na imepanga kuungana na kocha wake mpya Mserbia, Zaron Manojlovic kwa mara ya kwanza jijini Cairo kwa ajili ya kuanza kukisuka kikosi chake.

# HERSI AJIONDOA GSM

## ●●●Lengo ni kuitumikia vyema Yanga, shangwe zatawala baada ya...

**Na Saada Akida**

HERSI, Hersi Hersi ni kelele na mayowe ya furaha ya wanachama wa Yanga waliokuwa ukumbini wakimlaki Rais mpya wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said baada ya kupigiwa kura ya ndio.

Hersi amepita katika nafasi hiyo baada ya kuwa mgombea pekee na kupitishwa kwa kura ya 'NDIO' iliyopigwa na wanachama 805 ambao wanawakilisha matawi rasmi ya Yanga 161 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Hersi amekuwa Rais wa kwanza wa klabu hiyo baada ya kupitisha mabadiliko ya mfumo wa uendeshwaji kutoka kwa wanachama kwenda mfumo wa hisa ambapo hapo awali kiongozi wa juu alikuwa akitambulika kwa cheo cha Mwenyekiti.

Akizungumza baada ya kutangazwa mshindi, Hersi alisema kwa sasa atajitofautisha na kuwa mbali na mikataba ya GSM kwa kutekeleza kikamilifu majukumu yake ndani ya klabu hiyo.

"Ni kweli nimekuwa mwajiriwa wa GSM ila kwa sasa nitakuwa mbali na mikataba ya mdhamini huyo na kusimama upande wa klabu kwa kuhakikisha miaka minne ya uongozi wangu tunafanikisha yale mambo matano niliyosema katika kampeni zangu," alisema Hersi.

Alisema sasa atasimamia weledi mkubwa ikiwamo kushirikiana na viongozi wenzake katika kutimiza ahadi alizozitoa kwa wanachama.

"Yanga ni klabu kongwe, tunajivunia ukongwe lakini ni aibu kutokuwa na miundo mbinu, sasa nitasimamia suala la ujenzi wa uwanja wa watu 20, 000 na kwa tathimini niliyopiga, nina imani sehemu ya Kaunda inatosha.

"Katika miundo mbinu pia tutahakikisha ardhi iliyopo Kigamboni kujenga sehemu ya uwanja wa timu kufanya mazoezi lakini sehemu ya kituo cha kuendeleza soka la vijana na kuwapo kwa hosteli," alisema Hersi.

Aliongeza amejipanga kuitoa Yanga, katika mfumo wa kuendesha soka kizamani na kwenda kisasa, kusimamia vyema katiba yao katika kuendeleza pale walipoishia viongozi waliopita.

Alisema pia anahitaji kuimarisha uchumi wa klabu hiyo na kuifanya imara kwa kukuza vitega uchumi na kuifanya klabu hiyo kujiendesha kwa umahiri mkubwa.

"Jambo lingine ni kuhakikisha tunashinda mataji kwa msimu ujao kwa kufanikiwa kutetea mataji yetu yote kwa kushirikiana vyema na viongozi wenzangu tulioingia nao madarakani," alisema na aliongeza;

"Kujenga uimara wa timu zetu, vijana kwa kupata wachezaji ambao wataleta mchango kwa timu kubwa lakini nitaweka jitihada kwenye timu yetu ya wanawake, (Yanga Princess)," alisema Hersi.

Aliahidi ataimarisha ushirikiano kati ya klabu na wanachama, mashabiki na wadau wote wa soka ikiwamo kuleta mahusiano mazuri kwa taifa na kuhakikisha wanajenga maendeleo ya michezo nchini.

Mwenyekiti aliyemaliza muda wake, Mshindo Msolla aliwapongeza wajumbe wote aliofanya nao kazi na kuweka wazi haikuwa rahisi kwao kutokana na mazingira ya klabu.

"Miezi mitano ya kwanza tulifanya kazi katika mazingira magumu kwa sababu timu iliwahi kuzuiliwa hoteli kwa sababu haikuwa na fedha za kulipia, kipindi timu ikiwa Iringa. Nitakuwa Mwenyekiti mstaafu lakini pia sitakuwa nje ya Yanga kwa sababu mbali na Nesredine Nabi na Cedric Kaze, lakini nje ya benchi hili kuna watu wenye taaluma ya ukocha ambao ni Msolla na Mwinyi Zahera," alisema Msolla.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >